Jumanne Desemba 3, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii

epaper.ippmedia.com

www.ippmedia.com

ISSN 0856 • Na. 0581879

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

Nipashe digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0677 020 710 LIKE & FOLLOW US

UKURASA WA 4
RIPOTI MAALUM
**Msuguano** kijamii unavyoangamiza misitu ya mkoa

UKURASA WA 5
**Korti** yaahirisha kutoa hukumu shauri la Lissu



UKURASA WA 7
**Malori** yaegeshwayo barabarani yageuka kero Dar es Salaam

UKURASA WA 22
GUARDIOLA: MAN CITY ITAANZA UPYA

# Kaka wa Mwenyekiti CCM Mkoa achinjwa

• **Mwaka** jana mifugo yake ilikatwakatwa... *Ukurasa 3*



Rais Samia Suluhu Hassan akiongoza waombolezaji kutoa heshima za mwisho mbele ya jeneza lenye mwili wa aliyekuwa Mbunge wa Kigamboni na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda ya Afrika, Faustine Engelbert Ndugulile katika viwanja vya Karimjee, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Rais Samia: Tutawania tena nafasi ya Ndugulile WHO



UK. 2

# Nondo atupwa na watekaji, maswali matano yaibuliwa kwa Jeshi la Polisi

UKURASA 3

MICHEZO YANGA: MZUKA JUU LIGI YA MABINGWA UK.24 MAONI, UK.6

# Rais Samia: Tutawania tena nafasi ya Ndugulile WHO



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akifariji familia ya marehemu Dk. Ndugulile baada ya kuwasili katika viwanja vya Karimjee jana. **PICHA: IKULU**

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema Tanzania itaingia tena katika ushindani wa nafasi ya Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda ya Afrika.

Alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam alipoongoza wananchi na viongozi wa kitaifa na kimataifa kuaga mwili wa aliyekuwa Mbunge wa Kigamboni na Mkurugenzi Mteule wa WHO Kanda ya Afrika, Dk. Faustine Ndugulile.

Kiongozi huyo aliyefariki dunia Novemba 27 mwaka huu, alichaguliwa kwenye nafasi hiyo Agosti 28 mwaka huu na angeanza majukumu yake Februari 2025.

"Lakini niseme Dk. Faustine katika safari yake hii ya mwisho ameweka heshima kubwa kwa nchi yetu kwa kupata nafasi ile, na niseme kwamba Mungu amechukua amana yake, lakini kwetu sisi ni kwenda mbele.

"Tutaingia tena katika ushindani wa nafasi ile, tutatafuta mtanzania mwenye sifa zinazoweza kushindana na ulimwengu, tutaingia tena na tutaweka nguvu ileile ili kuweka heshima ya nchi yetu. Tunamshukuru sana Dk. Faustine kwa mchango aliotoa kwa taifa.

"Lakini kama tunavyoambiwa kwenye methali za Kiswahili, 'mwanadamu hupati unachotaka, unapata majaaliwa'. Tulichokuwa tunataka ni ndugu yetu huyu atuwakilishe katika shirika lile (WHO), awakilishe Tanzania, na Tanzania kupitia yeye itoe mchango kwa Afrika na dunia kwa ujumla katika fani ya afya lakini kwa Mungu hakutaka twende hivyo, akatupa jaala yake. Wanadamu tunapanga yetu lakini Mungu anapanga ya kwake," Rais alisema.

Watoto wa marehemu Dk. Ndugulile walisema wamepoteza mwanga wao, nguzo na shujaa wao kutokana na vitu alivyokuwa anavifanya kwa familia na jamii.

"Tulipata baba ambaye alikuwa shujaa na aliyetufundisha mambo mengi. Kimwili tumempoteza lakini kiroho tutaendelea kuwa naye," walisema Martha na Melvin.

"Baba alikuwa jasiri, mkarimu, mwenye akili na alipenda watu, nilipata baba... kwangu atabaki kuwa baba bora zaidi," alisema Melvin.

Askofu Msaidizi Jimbo Kuu Katoliki Dar es Salaam, Stephano Musomba aliyeongoza ibada ya kuaga mwili wa Dk. Ndugulile, alisema ili ukumbukwe ni lazima utende mema na kwamba ni vyema watu wajifunze namna ya kuishi na jamii.

"Hakuna atakayekusahau kutokana na matendo yako, hii ni safari ya kujifunza namna ya kuishi na watu, kusaidiana, kuhudumia, safari hii ni darasa ambalo limejaa elimu ya kutosha," alisema Askofu Musomba.

**SPIKA TULIA**

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alisema Dk. Ndugulile alikuwa miongoni mwa waliotoa mchango mkubwa katika kumfanyia kampeni kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU).

"Ninakushukuru sana Rais Samia kwa bidii kubwa uliyoweka kuhakikisha Dk. Faustine anashinda nafasi hii ambayo pamoja na kwamba ni kama tumekatizwa hivi, lakini imeongeza heshima kwa nchi yetu kuonesha uwezo wa wananchi wa Tanzania ambao unawaongoza.

"Mimi mwenyewe heshima ambayo nimeipata ya kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani, Dk. Faustine alikuwa sehemu ya watu ambao walifanya kampeni kwa bidii sana na sina shaka kwa sababu uchaguzi wake ulikuja mwaka mmoja baada yangu, alitumia ule uzoefu ambao wewe Rais ulitoa fursa ya yeye kushiriki katika kampeni, na alitumia uzoefu huo na sasa nchi yetu ikawa imepewa heshima hii.

"Sina shaka Mheshimiwa Rais kuwa jambo hili unalolifanya kwa bidii sana utaendelea kufanya hivyo kwa watanzania wengine wanaojitokeza lakini kwa sababu mimi na Dk. Ndugulile tulikuwa tunatoka upande wa Bunge la Jamhuri, tunakushukuru sana kwa ushirikiano ambao huwa unatupa kila wakati fursa hizi zinapojitokeza," alisema Dk. Tulia.

**WAZIRI MKUU**

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema amefanya kazi na Dk. Ndugulile na anatambua namna ambavyo amefanya kazi kubwa.

"Tukio hili si dogo, tangu tulipopata taarifa, tulipata mshtuko, binafsi ninatambua namna ambavyo nimefanya naye kazi kwa weledi mkubwa wakati wa utumishi wake, nimeshuhudia namna ambavyo amekuwa akishughulikia matatizo ya watu wa Kigamboni, amekuwa mtumishi katika serikali," alisema Majaliwa.

Rais wa Chama cha Madaktari Tanzania (MAT), Dk. Alex Msyoka, alisema wanamkumbuka Dk. Ndugulile kwa ujasiri wake hususani katika kipindi cha kupambana dhidi ya UVIKO-19, ambapo alisimamia taaluma yake kwa ufanisi, na kwamba alikuwa miongoni mwa wanataaluma wa kwanza kuanzisha Mpango wa Kudhibiti Ugonjwa wa UKIMWI Tanzania.

**JOSEPHAT GWAJIMA**

Akizungumza kwa niaba ya wabunge, Mbunge wa Kawe, Askofu Josephat Gwajima, alisema Mungu amempatia kila mtu kutimiza kazi yake na kwamba ni vyema kila mtu kuitimiza kwa kuwa muda ni mfupi.

**HALIMA MDEE**

Mbunge wa Viti Maalum, Halima Mdee alisema, "Mimi kama mwakilishi wa kambi ya watu wachache, ninamfahamu katika shughuli zetu toka mwaka 2010, alikuwa siyo mnafiki, alikuwa kama ana jambo lake kama ni nyeupe atasema nyeupe, kama ni bluu atasema bluu, alitumia muda wake kuwakilisha wananchi, alikuwa anasema kweli tupu, pasipo kujali itamgharimu vipi.

"Tuliomfuatilia alipata ajali za kisiasa kwa sababu ya kuzungumza ukweli, alisimamia anachokiamini, alikuwa mtii. Anatufundisha kwamba hutakiwi kuwa baridi au vuguvugu, inabidi uwe moto utimize ndoto.

"Watoto wanajua ni wa moto na sisi wanasiasa tulijua ni wa moto, hivyo tunaposimama katika jambo la ukweli tunatakiwa tuwe wa moto, ukiwa wa moto unasaidia nchi na kuinua taifa."

Mkurugenzi wa WHO, Kanda ya Afrika, Rebeca Masibiso, alisema Dk. Ndugulile alikuwa mwenye maono kwa ajili ya yale aliyokuwa akifanya, mbunifu, aliwajibika na ndio maana alifanikiwa kushawishi mkutano na kumchagua katika nafasi hiyo WHO.

Waziri wa Afya ya Congo Brazzaville, Gilbert Mukoki, alisema Dk. Ndugulile alivutia hisia za wajumbe wengi wa mkutano wa WHO, na kwa muda mfupi alifanya kampeni kwa ufanisi mkubwa na kuwashawishi wajumbe. Alimtaja "alikuwa mtu makini".

"Wakati tunajiandaa kumpokea kwenye nafasi yake mpya, tukapokea taarifa za kuhuzunisha. Alikuwa na maono ya kufanya mageuzi makubwa kwenye Kanda ya Afrika, maono yake yataendelea kuenziwa na tunaamini yatakuwa mwanga," alisema.

**BALOZI NCHIMBI**

Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, alisema Dk. Ndugulile alikuwa mfano wa kuigwa kwa kizazi cha sasa na kijacho kwa kazi alizofanya na alitoa wito kwa viongozi wote kuiga maisha yake ambayo yalijali maisha ya mtanzania wa kawaida, alijiepusha na ubinafsi na kutanguliza taifa mbele na kwamba ndio maisha ambayo kiongozi anapaswa kuishi.

Dk. Ndugulile alifariki dunia usiku wa kuamkia Novemba 27, mwaka huu India alikokuwa anapatiwa matibabu. Alikuwa mtaalamu wa afya, mwanasiasa mahiri na kiongozi wa mfano aliyetoa mchango mkubwa katika maendeleo ya sekta za afya, mawasiliano na usimamizi wa kimataifa.

Alizaliwa Machi 31, 1969 katika wilaya ya Mbulu, mkoani Manyara. Alipata elimu ya juu na kuwa miongoni mwa wataalamu wa kipekee waliochanganya taaluma ya tiba na sheria.

Alipata Shahada ya Udaktari wa Tiba (MD) mwaka 1997 na Shahada ya Uzamili ya Tiba (MMed) mwaka 2001 kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Mwaka 2010 alihitimu Shahada ya Uzamili ya Afya ya Umma (MPH) kutoka Chuo Kikuu cha Western Cape, Afrika Kusini, na mwaka 2022 alikamilisha Shahada ya Sheria (LL.B) kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT).

**SIASA, UONGOZI**

Dk. Ndugulile alijiunga na siasa mwaka 2010 alipochaguliwa kuwa Mbunge wa Kigamboni kupitia CCM na aliongoza jimbo lake kwa kujituma, akitekeleza miradi ya kuboresha miundombinu, afya na huduma za kijamii.

Mwaka 2007 hadi 2010 aliwahi kuwa Mshauri Mkazi wa Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC) Afrika Kusini, akitoa msaada wa kiutaalamu kwa nchi nyingine nyingi kama vile Angola, Msumbiji, Tanzania na Rwanda.

Oktoba mwaka 2017, Rais wa Tanzania wa wakati huo, Dk. John Magufuli, alimteua kuwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, akisimamia mipango muhimu ya kuboresha huduma za afya, hususani afya ya mama na mtoto.

Baada ya Uchaguzi Mkuu wa 2020, aliteuliwa kuwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari akiongoza kwa ubunifu, na kusisitiza matumizi ya teknolojia kuboresha maisha ya wananchi na kuimarisha uchumi wa kidijitali.

Agosti 27, 2024, Dk. Ndugulile alichaguliwa kuwa Mkurugenzi wa WHO Kanda ya Afrika, nafasi iliyompa heshima kubwa na Tanzania kwa ujumla.

Pia alikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Afya ya Bunge la Tanzania, Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Mabunge ya Kimataifa (IPU) Advisory Group Health na mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Mtandao wa Kamati za Afya za Bunge la Afrika (NEAPACOH), ameacha watoto wawili, Martha na Melvin Ndugulile.

Dk. Faustine Ndugulile atakumbukwa kama kiongozi shupavu aliyewakilisha Tanzania kwa heshima katika majukwaa ya kitaifa na kimataifa, akiwa mfano wa kuigwa kwa uadilifu na bidii. Mchango wake katika sekta ya afya, mawasiliano na usimamizi utaendelea kuishi milele.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms / WhatsApp : +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
Tarehe 03/12/2024

## TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumanne tarehe **03-12-2024** kampuni ya **HAINAN INTERNATIONAL LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **IRINGA-Ruaha** kuelekea **DAR ES SALAAM**, gari hilo lenye namba za usajili:

**T 176 DFN / T 171 DFN.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 18.00**
**Upana - mita 2.80**
**Kimo - mita 5.00**

3. Njia itakayotumika: **IRINGA-Ruaha** hadi **DAR ES SALAAM** kupitia **MOROGORO ROAD.** Gari itasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

182790

HABARI KITAIFA

# Kaka wa Mwenyekiti CCM Mkoa achinjwa

**Na Waandishi Wetu,** MOSHI

ISAACK Mallya, ambaye ni kaka wa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Kilimanjaro, Patrick Boisafi, ameuawa kikatili kwa kucharangwa mapanga kichwani na shingoni baada ya kuvamiwa nyumbani na watu wasiojulikana.

Mallya, mkazi wa kijiji cha Umbwe Onana, Kobosho, wilayani Moshi, aliuawa jana saa mbili asubuhi.

Kamanda wa Polisi mkoani humo, Kamishna Mwandamizi Msaidizi (SACP) Simon Maigwa alithibitisha kuuawa kwa mtu huyo, huku akieleza kwamba chanzo cha mauaji hayo hakijajulikana.

"Ni kweli tukio hilo limetokea Desemba 2 mwaka huu katika Kijiji cha Umbwe Onana. Jeshi la Polisi linafuatilia kuona chanzo cha tukio hilo.

"Tunawaomba wananchi waache kuchukua sheria mkononi ili kupunguza mauaji yasiyo na hatia. Lakini niseme tu kwa sasa mwili wa marehemu umehifadhiwa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kaskazini (KCMC)," alisema.

Akizungumzia tukio hilo kwa njia ya simu, Mwenyekiti wa CCM, Kilimanjaro, Boisafi, alikiri marehemu Isaack Mallya, ni ndugu yake, kwa maana ya mtoto wa baba mkubwa.

"Ni ndugu yangu, ni mtoto wa baba yangu mkubwa, tumeishi wote, mji mmoja na mahali alipouawa, ndipo nimekulia hapo. Ni jambo la kikatili sana limefanyika katika jamii.

"Hata kama mtu ni mkorofi au nini, kitu kilichofanyika kinakemewa na kila mtu, yaani jambo lililofanyika ni la aibu, mtu kuamua kuchukua uamuzi wake kwenda kumuua mtu, tena nyumbani kwake.

"Kama walikuwa wanamdai, wangesema tungelipa, lakini kitu walichokifanya, kusema ukweli ni ukatili. Tunakemea jambo hili na lisijirudie kwa watu wengine, ni jambo linalosikitisha sana, kwani linajenga hofu hasa kipindi hiki ambacho tunaelekea sikukuu za mwisho wa mwaka," alisema.

Boisafi aliongeza, "Matukio haya yanayotokea, yanatisha hata wale ndugu zetu na marafiki zetu ambao watasafiri kutoka maeneo mbalimbali nchini na nje ya nchi kuja Kilimanjaro.

"Mambo haya yanatia doa Mkoa wa Kilimanjaro na jamii yote inayotuzunguka. Lakini ninaamini Jeshi la Polisi litafanya bidii kuchunguza matatizo yaliyotokea na kuwatafuta waliohusika na jambo hili ili hatua za kisheria zichukue mkondo wake."

**WALIANZIA MIFUGO**

Mwenyekiti huyo wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro alisema mauaji hayo ya kaka yake yamemsikitisha, akikumbusha kuwa, "Kipindi cha nyuma kuna mifugo iliuawa, walikwenda kukatakata ng'ombe wake, inawezekana wakati huo ndio walikuwa wakimtafutia 'timing' (kumvizia), ikawa tofauti.

"Maana muda ambao nimepata habari ni kipindi cha asubuhi, ambapo kwa kawaida huwa anahangaika na mifugo yake, halafu baadaye anakwenda kanisani," alidai.

Ndugu mwingine wa marehemu Isaack, ambaye ni mfanyabiashara maarufu katika Mji wa Moshi, Baraka Mallya, maarufu Fresh Coach, alisema: "Huyo aliyeuawa ni ndugu yangu, yaani ni tukio la kinyama kabisa kuwahi kutokea pale kijijini.

"Boisafi na huyo Isaack (marehemu), ni mtu na kaka yake. Ni mtu wa karibu sana na familia hiyo, Boisafi amekulia kwenye familia ya baba yake na marehemu Isaack."

Mmoja wa majirani, Manka Kipesa, ambaye ni mfanyabiashara wa ndizi, alisema majira ya asubuhi alifika katika eneo hilo kwa ajili ya ununuzi wa ndizi mbichi, baada ya kutoka katika nyumba nyingine na ndipo aliposhuhudia ukatili huo.

"Nilifika nyumbani hapo kwa ajili ya kutaka ndizi baada ya kutoka nyumbani nyingine kununua, nimefika hapa nikamkuta akichuruzika damu, ndipo nilipopiga kelele na majirani wakaja ingawa alipoteza maisha muda huohuo kabla ya kukimbizwa hospitalini," alidai.

Nipashe
WhatsApp Chaneli
Skani hapa kutembelea chaneli yetu

# Nondo adaiwa kutupwa ufukweni, hoja tano zaibuliwa Jeshi la Polisi

**Na Halfani Chusi**

ABDUL Nondo amepatikana akidaiwa kutupwa ufukweni. Chama cha ACT Wazalendo kimehoji maswali matano kwa Jeshi la Polisi kufuatia madai ya kutekwa kwa Mwenyekiti wake huyo Ngome ya Vijana Taifa.

Makamu Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo Bara, Isihaka Mchinjita, akiwa katika Hospitali ya Aga Khan, jijini Dar es Salaam jana alikomtembelea kumjulia hali, alidai Nondo amepigwa na kuumizwa. Kwa hali aliyokuwa nayo, hakuwa na uwezo wa kuzungumza vizuri.

Alisema Nondo alimsimulia kwa shida kilichojiri baada ya kutekwa juzi alfajiri kwenye Stendi ya Mabasi ya Magufuli; kwamba alifungwa kitambaa cheusi na kupigwa sana huku akitishiwa kuuliwa.

"Maelezo yake ni kwamba, alipotolewa pale Stendi ya Magufuli, alifungwa kitambaa, hivyo hakuwa anaona. Baada ya hapo amekuwa akipigwa muda mrefu, baadaye walisitisha kwenye eneo ambalo halifahamu kisha alitupwa pale Coco Beach ambako walimfungua kitambaa na pingu na baadaye akabaini yuko eneo hilo na akaomba msaada," alisimulia Mchinjita, kama alivyodai kuelezwa na Nondo.

Alipoulizwa kuhusu alichokuwa akiambiwa na wanaotajwa "watekaji", Mchinjita alisema, "Maelezo anayatoa ni kwamba alipigwa na alikuwa kwenye kitisho cha kifo na yeye alipopelekwa pale Coco Beach na pale baharini alijua ni hatima yake kwa sababu alikuwa amefungwa na wakamwacha kwenye eneo hilo, lakini baadaye akatishwa tu kwamba akikamatwa tena, basi hawatomwachia."

Mchinjita alidai Nondo alikutwa eneo hilo saa nne na nusu usiku wa kuamkia jana ndipo wasamaria wema walimchukua na kumpeleka makao makuu ya chama hicho Magomeni, wilayani Kinondoni kisha kukimbizwa hospitalini.

Alisema kuwa alipomtazama, aliona ameumizwa maeneo ya miguuni, kifuani, mgongoni na mikono yake ilikuwa inaonesha ilifungwa kwa muda mrefu. Imevimba.

"Madaktari wamesema taarifa ya uchunguzi ya awali hajavunjika, waendelea na matibabu lakini wametuambia watatoa taarifa kesho (leo) baada ya madaktari bingwa kuja, lakini kwa sasa wamekwenda kumlaza katika chumba cha upasuaji," alidai Mchinjita.

Alisisitiza kupatikana kwa taarifa za kutekwa kwake mapema na hata kugundua gari lililotumika kufanikisha utekaji, kumesaidia kupatikana haraka kwa kuwa wapo vijana wengi waliotekwa nchini na hawajapatikana.

Kiongozi wa Chama mstaafu, Zitto Kabwe alisema wakiwa mkoani Kigoma na Nondo wakati wa kampeni za uchaguzi uliokamilika Novemba 27, mwaka huu, hakuwahi kutishwa kwa namna yoyote ile.

Aliongeza kuwa hakufanya jambo lolote baya ambalo pengine linaweza kuwa sababu ya kutekwa kwake huku akisisitiza atakapopata nafuu atasimulia ili kupata funzo la namna ya kukabiliana na matukio hayo.

**MASWALI MATANO**

Naibu Katibu wa Ngome ya Vijana vya chama hicho, Ruqayya Nassir amelitaka Jeshi la Polisi kujibu maswali matano, ikiwamo kueleza zile pingu zilizoanguka na kuokotwa na mashuhuda katika tukio hilo ni za nani kwa kuwa haziuzwi kama karanga wala njugu?

Pili; amelitaka jeshi hilo litaje hatua lilizochukua kuhusiana na taarifa za awali kuhusu aliyemtaja kwa jina kuwa ndiye mmiliki wa gari lililotumika kumteka Nondo.

Hoja nyingine ya chama hicho ni kutaka kujua hatua zilizochukuliwa dhidi ya Kituo cha Polisi Gogoni ambako inadaiwa gari lililotumika katika utekaji ni la kituo hicho.

"Je, mpaka sasa jeshi limewabaini ni polisi waliomteka, kumpiga na kumtelekeza Nondo?" alihoji Ruqayya na kumtaka Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Camillus Wambura kutoa majibu aliyoyaita "yenye mashiko kutokana na suala hilo".

The Guardian Limited

VACANCY

**Sales Freelancer**

**The Guardian Limited** is looking for self driven sales Freelancer to join our **advertising** Sales Team in **Dar es Salaam, ( Moshi, Arusha, Tanga, Morogoro, Iringa, Mwanza and Zanzibar)**

**Responsibilities**

- Be responsible for aggressive development of new clients and growing existing business.
- Proactively develop new business avenues
- Devise and monitor business plans to ensure substantive sales
- Develop strategic solutions that meet the unique needs of each client

**Qualifications**

- The position requires someone who can deliver the set targets within deadlines under competitive working environment.
- Applicants need to be highly organized, self-motivated with a positive attitude, and can thrive on setting and reaching new goals.
- Holders of a University degree or Diploma in Business Administration
- Experience in Sales and Marketing is an added advantage

**NOTE: This is a commission Based Position**

182777

**Please send your application via Email to vacancy@guardian.co.tz before 15th December, 2024.**

RIPOTI MAALUMU

# Matukio ya msuguano wa kijamii yanavyoangamiza misitu ya mkoa

- Mikasa ya ulevi kazini, kuchomeana moto
- Urinaji asali usiozingatia vigezo na masharti
- TFS: Hasara bil. 400/-, matukio 138, hekta 112,000

**Na Elizabeth John,** NJOMBE



Matukio ya moto katika misitu yanatajwa kutishia uchumi wa mkoa wa Njombe.

CHUKI, visasi, dhuluma, hila, wivu wa maendeleo, urinaji asali na kilimo kando ya vyanzo vya maji, maarufu vinyungu, ni chanzo cha matukio mengi ya moto katika misitu ya Njombe, uongozi wa mkoa huo umethibitisha.

Kwa mujibu wa Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), mkoa wa Njombe ulioanzishwa rasmi mwaka 2012, unakadiriwa kuwa na hekta za misitu 664,720.83. Kati yake, misitu ya asili ina ukubwa wa hekta 263,320.83 na ya kupandwa ina ukubwa wa hekta 401,400. Misitu hiyo inachukua asilimia 31.39 ya ardhi yote ya mkoa huo.

Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2020/21 hadi 2022/23 kulikuwa na matukio ya moto 138 katika misitu ya mkoa huo yaliyoteketeza hekta 112,299.01 za miti zenye thamani ya Sh. 400,850,754,459.16 (bilioni 400.851/-).

Mchanganuo wa TFS unaonesha kuwa kati ya matukio hayo, Halmashauri ya Wanging'ombe ilikuwa na matukio ya moto 24 yakiteketeza hekta 446.8 zenye thamani ya Sh. 5,495,466,912 Halmashauri ya Ludewa ilikuwa na matukio 35 yaliyoharibu hekta 90,832.5 zenye thamani Sh. 142,512,570, Makete ilikuwa na matukio 22 yaliyounguza hekta 3,993.51 zenye thamani Sh. 74,545,560,661.26.

Halmashauri ya Mji wa Makambako ilikuwa na matukio 10 yaliyoteketeza hekta 49.6 zenye thamani ya Sh. 925,866,708, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ilikuwa na matukio 31 yaliyounguza hekta 6,381.6 zenye thamani ya Sh. 119,533,872,003 na Halmashauri ya Mji Njombe ilikuwa na matukio 16 yaliyoharibu hekta 10,573 zenye thamani Sh. 197,362,675,477.50.

Kwa mujibu wa TFS, mkoa wa Njombe mwaka 2023/2024 ulikuwa na matukio ya moto 51 yaliyoteketeza hekta 4,481.49 zenye thamani ya Sh. 5,692,025,943.50.

Mbali na kuchangia mabadiliko ya tabianchi, uchomaji moto misitu pia unatajwa kusababisha umasikini kwa wananchi wanaotegemea kilimo biashara (kilimo cha miti).

Baadhi ya wakazi wilayani Njombe waliozungumza na mwandishi wa habari hii, wanasema hakuna sheria kali ambayo inambana mwananchi moja kwa moja endapo atabainika kuchoma moto na kuunguza misitu.

"Ninadhani haipo, kama ingekuwapo sheria kali inayombana, kama vile kufungwa jela miaka kadhaa na wananchi wenzake wanakasikia 'jamani fulani aliyechoma moto ukaunguza milima na milima, amehukumiwa kifungo gerezani, ninaamini wengi wangejifunza. Lakini, hivi sasa unaona anayeunguza hana hata kitu chochote cha kulipa," anashauri Twiluma Mathias, mkazi wa wilayani Njombe.

Aneth Mwalongo, mkazi wa wilaya ya Njombe, anasema kuwa kutokana na kuwapo matukio mengi ya uchomaji misitu, baadhi ya watu wameacha kupanda miti. Wanahofia kupata hasara.

"Msitu ukishaungua, ninakula hasara. Hivyo, itafika wakati hakutakuwa tena na mbao huku kwetu kwa sababu wengi wanaunguliwa miti hiyo ya mbao ikiwa midogo ya miaka miwili, mitatu hadi mitano," Aneth analalama.

Mkazi mwingine wa wilayani Njombe, Bushery Kilasi, anasema kuwa baadhi ya wanaochoma moto misitu, wanafanya hivyo kwa makusudi kutokana na chuki waliyonayo.

"Hivi ni vita baridi na itakuwa ya moto zaidi tuendako. Mtu anachoma makusudi na hana shida na ikitokea amekamatwa kesi inaishia ofisini kwa watendaji, mambo yanaisha huko na wewe (mkulima/mwekezaji) tayari umepata hasara," anaonya Kilasi.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Kifanya, Halmashauri ya Mji wa Njombe, wilayani Njombe, Bariki Kabelege, anasema wamekubaliana kuwa na sheria ndogo zinazoelekeza kutoa fedha Sh. 20,000 kwa mtu yeyote atakayebaini kuwapo moto katika eneo lolote hata kama haujaanza kuleta madhara katika msitu husika. Kwa atakayesababisha tukio la moto, atapigwa faini ya fedha Sh. 50,000.

"Tumeamua kuwa na utaratibu huu kwa sababu kasi ya mashamba kuungua ni kubwa kwetu. Kuna matukio mengi ya moto wakati wa kuandaa mashamba, maarufu vinyungu.

"Kuanzia mwezi Julai mwaka huu mpaka sasa (mwezi uliopita), ni hekta nyingi. Lakini ni zaidi ya hekta 200 zimeteketea ambazo zilikuwa na mazao, kitu ambacho kinarudisha nyuma maendeleo.

"Ni hasara kubwa kwa wananchi wenyewe, wawekezaji wa nje wanaokuja kuwekeza na wafanyabiashara wengine ambao kazi yao si kupanda miti au kuzalisha miti, bali kuchakata au kupata mazao ya misitu," anasema Kabelege.

Diwani wa Kifanya, wilayani Njombe, Nolasco Mtewele, anasema pamoja na kuwapo sheria ndogo zinazoelekeza hatua za kukabiliana na moto msituni, hazitekelezwi vizuri na watendaji wa serikali.

"Ninaomba vijiji vyote vinavyozunguka kata ya Kifanya vihakikishe kwenye suala la moto, vinaweka kipaumbele sana kwa sababu uchumi wetu tunaonekana tupo vizuri kutokana na misitu ambayo tunapata mbao," anasema Mtewele.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kifanya, Alberto Mkalawa, anasema wanazo sheria ndogo za kijiji zinazoelekeza, "ukihitaji kusafisha shamba kwa kuchoma moto, ni lazima wawapo watu wasiopungua 10 wakati wa uchomaji moto".

Hata hivyo, Mwenyekiti Mkalawa ana angalizo lenye ushuhuda, akisema, "Tukaja kugundua changamoto kwamba mwenye kibali cha kuandaa shamba, akishapata watu 10 wa kumsaidia kudhibiti moto, anabeba pombe anakwenda nayo huko shambani.

"Madhara yake ni kwamba watakunywa ile pombe, hawatakuwa makini kuzingatia ule moto namna walivyochoma lile shamba, na isivyo bahati inatokea wanashindwa kudhibiti moto, hivyo kuangamiza msitu jirani na shamba husika."

Mhifadhi wa Misitu Mwandamizi wa TFS Wilaya ya Njombe, Audatus Kashamakula, anasema uchomaji misitu Njombe unasababishwa na mambo mengi yanayojumuisha visasi na chuki, urinaji asali na uandaaji mashamba.

Kashamakula anataja vyanzo vingine vya matukio ya moto misituni Njombe ni uchomaji mkaa na uchomaji mashamba ya miti kwa makusudi ili kuwakomesha wamiliki wa mashamba hayo ikiwa kuna migogoro ya kifamilia. Hasara huwakumba hata wasiohusika na mgogoro husika kwa kuwa moto huunguza hadi mashamba yaliyo jirani.

"Wananchi wengi wa Njombe wana utamaduni wa kizamani wa kuandaa mashamba kwa kuchoma moto pasi na mikakati mizuri ya kuudhibiti," anasema Kashamakula.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, anaelekeza hatua za haraka zichukuliwe ili kukabiliana na majanga ya moto yanayosababisha hasara kubwa kwa jamii na taifa.

Maelekezo yake kwa watendaji walio chini yake ni kwamba kila wilaya iweke mikakati ya kuvifikia vijiji vyote kwa ajili ya kutoa elimu ya kukabiliana na matukio ya moto yanayoteketeza misitu.

"Lazima tufanye kazi kwa pamoja ili tuje na majawabu kwenye suala la moto katika mashamba yetu ya misitu, ni hasara ya mabilioni. Hatuwezi tukaliacha hili jambo, mapato ya mkoa wa Njombe kwa sehemu kubwa yanategemea ushuru kwenye mazao ya misitu; shamba au mbao, magogo, mabanzi, mirunda, mkaa na guzo. Hivyo ni lazima tujue kwamba uchumi wetu upo hapa.

"Mtu anapokwenda kuandaa nusu ekari ya shamba la mahindi, akichoma kwa ajili ya kusafisha shamba, kuna mtu mwingine huku anapoteza ekari 500 za miti.

"Hivyo, ni lazima huyu mtu ajue hii hasara atakayokuwa ameisababisha, kuna watu wanapata kiharusi, kuna watu huko wanachanganyikiwa kwa sababu ya tatizo hili," anaonya Mtaka.

Ofisa Ukaguzi wa Usalama wa Moto Mkoa wa Njombe kutoka Jeshi la Zimamoto, Hilary Kobero, anasema wanaendelea kutoa elimu ya uandaaji mashamba pasi na kusababisha hasara.

"Miongoni mwa njia ambazo wanapaswa kuzifuata kwelikweli ni zile sheria ndogo ambazo zimewekwa katika mamlaka za serikali za vijiji. Sheria ziko wazi, zinasema muda, hali ya hewa ambayo inapaswa ifuatwe lakini pia na idadi ya watu wanaopaswa wawapo wakati wa kuwasha moto," anasema Mkaguzi Kobero.

Anasisitiza kuwa wananchi wakiona upepo ni mkali, hawapaswi kuchoma moto mashamba yao siku hiyo hata kama wamepewa kibali.

Mkaguzi Kobero pia anatoa rai kuchongwa barabara za kutosha kutoka shamba moja hadi lingine, ziwe na upana na mita sita, hasa kwa mashamba ya miti ili kusaidia kuzuia moto kutoka shamba moja kwenda lingine.

Vilevile, mkaguzi huyo aliwataka maofisa kilimo mkoani Njombe kutoa elimu kwa wakulima ili watumie njia mbadala kuandaa mashamba. Waache kuandaa mashamba yao kwa kuchoma moto.

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*

HABARI KITAIFA

# Mahakama yaahirisha kutoa hukumu shauri la Tundu Lissu

**Na Elisante John, SINGIDA**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Singida imeahirisha kutoa hukumu ya shauri dogo lililofunguliwa na Wakili Tundu Lissu kupinga kesi namba 19525 mwaka 2024 inayomhusu Askofu Machumu Kadutu wa Kanisa la Ufufuo na Uzima la jijini Dar es Salaam kwa kuwa hukumu haijakamilika.

**"Wangapi nyumbani mna panga...? Sasa mimi ninawaambia hivi; kama kupitia polisi... kama wamerudia tena katika uchaguzi ili wapitishe wanavyotaka wao, haki ya Mungu safari hii haya majembe yatakuwa na matumizi mengine... wakiwananii na nyie mnafanyaje? Mnawananiii..."**

Askofu huyo anashtakiwa kwa tuhuma za kutamka maneno ya uchochezi akiwa kwenye mkutano wa hadhara wa siasa uliofanyika kata ya Ibaga, wilaya ya Mkalama, mkoani Singida.

Katika shauri hilo dogo, Lissu anaomba mahakama hiyo itupilie mbali shauri dhidi ya mteja wake kwa madai kuwa kesi hiyo haina mashiko.

Akiahirisha kesi hiyo jana hadi Desemba 16 mwaka huu, Hakimu Mkazi Mkuu Mfawidhi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Singida, Allu Nzowa, alisema hukumu haijakamilika, hivyo mahakama inaendelea kuandaa.

Katika shauri hilo la jinai namba 19525 la mwaka 2024, Askofu Kadutu, kama ilivyoelezwa kwenye hati ya mashtaka, anadaiwa kutamka maneno hayo ya uchochezi alipokuwa anahutubia wananchi katika mkutano wa hadhara uliofanyika Juni 3, mwaka huu katika kijiji cha Ibaga, wilayani Mkalama.

Ilidaiwa mahakamani huko na Wakili wa Serikali Almachius Bagenda kuwa maneno aliyoyatoa mshtakiwa ni kosa kisheria na yanaweza kujenga chuki ya wananchi dhidi ya askari na serikali yao.

Wakili Bagenda alidai kuwa siku hiyo ya tukio, mshtakiwa alitamka maneno: "... naweza kukosea njia wakati wa kwenda lakini huwezi kukosea njia wakati wa kurudi, mmeshaifahamu njia, walichofanya 2019 hakitajirudia... wangapi nyumbani mna majembe, wangapi mna visu nyumbani?

"Wangapi nyumbani mna panga...? Sasa mimi ninawaambia hivi; kama kupitia polisi... kama wamerudia tena katika uchaguzi ili wapitishe wanavyotaka wao, haki ya Mungu safari hii haya majembe yatakuwa na matumizi mengine... wakiwananii na nyie mnafanyaje? Mnawananiii..."

Alidai maneno hayo yaliyotamkwa katika soko la zamani, eneo la Madukani, kijiji cha Ibaga, ni kinyume cha sheria za nchi.

Kabla ya kuahirishwa kesi hiyo, Wakili Hemedi Kulungu, anayemtetea mshtakiwa, alisema Lissu hakuwa mahakamani jana kutokana na kuwa kikazi nje ya mkoa wa Singida, anakoshiriki kikao cha Kamati Kuu ya Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), jijini Dar es Salaam.

Jopo la Mawakili wa Serikali linaongozwa na Almachius Bagenda, akisaidiana na Nehemia Kilimhana na Michael Martin wakati Lissu anasaidiwa na Hemedi Kulungu.





Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Yanayokwaza mkakati kutokomeza VVU na UKIMWI yashughulikiwe

**KATIKA** toleo letu la jana, tulikuwa na habari kuhusu maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Philip Mpango na Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman wakija na mambo kadhaa ambayo ni kikwazo katika kufikia lengo la kutokomeza UKIMWI kufikia mwaka 2030.

Akiwa mjini Songea, mkoani Ruvuma juzi, Dk. Mpango alitaja vikwazo hivyo vinajumuisha jamii kuwa na mtazamo hasi dhidi ya walioambukizwa virusi hivyo, hata kuchangia kurudisha nyuma jitihada za kupambana na UKIMWI.

Mtazamo hasi, kama ilivyofafanuliwa na Makamu wa Rais, huwafanya wahitaji kushindwa kupata huduma kwa kuonekana kuwa hawastahili na hivyo kutengwa, huku akionya unyanyapaa husababisha woga unaoathiri upimaji wa hiari na upatikanaji huduma nyingine kama za unasihi pamoja na ARV kwa wale wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (VVU).

Kuna angalizo lingine la Makamu wa Rais kwa vijana, kwamba wanapaswa kujitambua, kujithamini na kutunza maisha yao kwa kujikinga na maambukizi mapya ya VVU kwa kuwa kasi ya maambukizi katika kundi hilo inaonekana kuwa kubwa. Takwimu za hali ya UKIMWI nchini zinaonesha kundi la vijana, hasa wa kike, liko katika hatari zaidi ya kupata maambukizi mapya ya VVU.

Maambukizi mapya, kama ilivyoelezwa na Makamu wa Rais, yanachochewa zaidi na mazingira na tabia hatarishi hususan ulevi uliopindukia, ngono zembe, kuwa na wapenzi wengi na matumizi ya dawa za kulevya.

Matokeo ya utafiti wa viashiria vya VVU na UKIMWI uliofanyika mwaka 2022/23, yanaonesha maambukizi mapya miongoni mwa watu wazima wenye umri kuanzia miaka 15 ni watu 60,000 kwa mwaka. Kiwango cha ushamiri wa VVU kitaifa ni asilimia 4.4 ambapo jumla ya watu 1,548,000 wanaishi na VVU.

Ingawa kiwango cha ushamiri wa VVU kwa wenye umri kuanzia miaka 15 na zaidi kwa upande wa Zanzibar ni cha asilimia 0.4, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman, anataja changamoto zinazohusiana na haki za binadamu katika upatikanaji huduma za UKIMWI zinachangia kwa kiasi kikubwa kuzorotesha juhudi za serikali na ulimwengu kwa ujumla katika kumaliza tatizo la UKIMWI.

Akiwa mkoa wa Kusini Pemba juzi, Othman aliungana na Dk. Mpango kukemea unyanyapaa na watu kulazimishwa kupima, akionya kuwa hali hiyo husababisha watu kukosa na kuogopa kuzifikia huduma za kujikinga na VVU pamoja na za matibabu kwa wanaoishi na VVU.

Othman pia alikosoa tabia ya baadhi ya mashirika na taasisi kuwalazimisha wafanyakazi wao hasa inapotokea haja ya kuongezwa mikataba, kupimwa kwa lazima, jambo ambalo ni kinyume cha sheria za afya Zanzibar.

Nipashe, tukiwa wadau katika mapambano hayo, tunaungana na serikali na Shirika la Afya Duniani (WHO) kuhimiza kuwapo mikakati endelevu kuhakikisha kila mdau anashiriki katika mapambano dhidi ya UKIMWI, ikiwamo kuondoa unyanyapaa na kuhakikisha waliogundulika kuwa na maambukizi wanapatiwa matibabu.


Pamoja na taarifa zilizotolewa hivi karibuni kuonesha kuna kushuka kwa maambukizi ya VVU nchini, Nipashe tunaona kuna umuhimu mkubwa wa kuongeza nguvu katika mapambano dhidi ya janga hilo. Elimu kwa umma inapaswa kuendelea kutolewa kwa makundi mbalimbali hasa ya vijana na wanawake ambao wako katika hatari kubwa zaidi ya kupata maambukizi.

Kwa kuwa kundi la vijana ambalo serikali imeweka wazi liko katika hatari zaidi, ni vyema wadau wa afya wakatilia mkazo zaidi kwa kuwaelimisha kuhusu hatari ya ugonjwa huo. Elimu inapaswa kutolewa katika shule, vyuo vya elimu ya juu, migodini na maeneo ya uvuvi ambako kuna hatari zaidi ya maambukizi kitaifa.

Vijana katika maeneo hayo wanakuwa hatarini kupata maambukizi kwa sababu ya kuwa na tamaa ya kupata vitu vizuri.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Jihusishe kulinda elimu ya msichana

**TANZANIA** inaendelea kupiga hatua kwenye sekta ya elimu kwa kuweka mikakati mingi mfano; kuanzisha, kuongeza shule za msingi na sekondari, kugharamia elimu kuanzia msingi hadi sekondari na kujenga shule za sayansi kwa wasichana.

Moja ya malengo ya kuwekwa kwa mikakati hiyo ni kutaka kila mtoto awe wa kutoka familia maskini au tajiri, apate elimu.

Hatua hiyo inatokana na ukweli kwamba elimu ndio msingi mkuu wa kumwezesha mtu kuwa na uelewa wa kutosha, kwani elimu ndio inayomfanya aweze kujitambua na kujimiliki mwenyewe.

Vilevile, elimu inamfanya mtu aweze kuzikabili changamoto zinazomzunguka katika maisha yake ya kila siku na pia kuweza kuyatawala na kuyatumia mazingira yake ili kuboresha maisha yake.

Hata hivyo, kumekuwapo na wingi wa mimba za wanafunzi na ndoa za utotoni kwa kwenye baadhi ya maeneo ambazo kwa namna moja au nyingine ni kikwazo kwa maendeleo yao kielimu kwa watoto wa kike.

Kwa mfano, ndani ya mwezi mmoja wanafunzi wa shule za msingi na sekondari 194 walibainika kupewa mimba na kukatishwa masomo yao katika wilaya ya Momba mkoani Songwe.

Hayo ni kwa mujibu wa mkuu wa mkoa huo, Daniel Chongolo, wakati akizungumza na wananchi katika kijiji cha Chiwanda wilayani humo hivi karibuni na kuwataka wazazi na walezi kutomalizana kimya na wahalifu.

Wilaya moja idadi ya wanafunzi waliopata mimba ndani ya mwezi mmoja ndio hiyo. Idadi kama ikiwa katika kila wilaya kwa nchi nzima yenye wilaya zaidi ya 100 hali itakuaje?

Ipo haja kwa jamii kulinda maendeleo ya elimu ya mtoto wa kike kwa kushirikiana na serikali kukikabiliana na tatizo la mimba hizo, ambazo zimekuwa ni kikwao cha maendeleo ya elimu kwa mtoto wa kike.

Mimba zinasababisha upatikanaji wa elimu kwa wote kukabiliwa na tatizo na huenda linazidi kuwa kubwa iwapo jamii itajiweka pembeni kwenye vita hiyo ya kutokomeza ukatili huo wa kijinsia.

Katika kukabiliana na tatizo hilo, maofisa elimu na ustawi wa jamii wajitahidi kuwa wabunifu kwa kuanzisha klabu rika, katika shule na kwa shule ambazo klabu hizo zipo, basi ziimarishwe.

Ikumbukwe kuwa wasichana wanaokatisha masomo na uharibu maisha yao, wamo ndani ya jamii na ni sehemu ya jamii, hivyo ni muhimu jamii ihusike katika kukomesha mimba na ndoa za utotoni.

Wazazi na walezi nao hawana budi kuzungumza na watoto wao na kuwaelekeza, kuwafundisha maadili mema wakiwa wadogo ili yawe ngao yao ingawa inawezekana wakayaacha, lakini ni muhimu kutimiza wajibu katika malezi. Elimu ya makuzi ni ya muhimu, kwani ni mojawapo ya njia ya kuwaepusha tamaa, ambazo mwisho wake zinaweza kusababisha wapate mimba na kukatisha masomo bila kutarajia.

Suala la malezi pia linawagusa walimu, kwani wao ndio wanaokaa na wanafunzi muda mrefu na wanaona mabadiliko ya wanafunzi kitaaluma, kitabia, kimwenendo na kimaadili.

Walimu wasiwe sehemu ya tatizo la mimba, kwani baadhi yao huwa wanatuhumiwa kufanya mapenzi na wanafunzi wao, kitendo ambacho kinaonyesha kuna mmomonyoko wa maadili.

Kwa ujumla ni kwamba kila atakayebainika kujihusisha na mapenzi na wanafunzi, sheria ichkue mkondo wake bila kujali ni nani. Awe mwalimu, ndugu wa mwanafunzi au mtu yeyote, wote wanapaswa kuchukulia hatua za kisheria ili kukomesha vitendo hivyo katika jamii.

Wanafunzi wa kike kama walivyo wa kiume, nao wana ndoto zao walizojiwekea katika elimu, hivyo kuwapa mimba ni sawa na kuwaharibia ndoto hizo hata kama kwa sasa kuna utaratibu wa wao kurudi shuleni kuendelea na masomo baada ya kujifungua.

# NECTA yashtushwa na takwimu ukataji miti

**Na Romana Mallya**

BARAZA la Mtihani Tanzania (NECTA) limehamasisha jamii kupanda miti katika maeneo yao kwa kuwa takwimu za kidunia zinaonesha kasi ya ukataji miti ni kubwa tofauti na upandaji.

Katika kuleta hamasa hiyo kwa jamii, baraza hilo limepanda zaidi ya miti 2,000 katika shule tano za msingi zilizoko jijini Tanga, kama sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja.

Akizungumza wakati wa upandaji miti uliofanyika katika Shule ya Msingi Mleni iliyoko, kata ya Mzizima, jijini humo, Katibu Mtendaji wa Baraza hilo, Dk. Said Mohamed, alisema suala la upandaji miti ni endelevu katika kuunga mkono jitihada za utunzaji mazingira.

Alisema takwimu za kidunia zinaonesha kasi ya ukataji miti ni mkubwa tofauti na upandaji, hivyo kampeni hiyo imelenga kuhakikisha wanahamasisha wananchi kushiriki katika utunzaji mazingira.

"Malengo ni ifikapo mwaka 2030 kidunia tuwe tumepanda miti takribani trilioni moja, hivyo na sisi NECTA tumeanza kuunga mkono juhudi hizo kwa kupanda miti katika shule zetu nchi nzima.

"Sisi ni sehemu ya wadau ambao tunaongoza kwa kutumia makaratasi ambayo yanatokana na miti," alisema katibu huyo.

Mwakilishi wa Katibu Tawala wa Mkoa wa Tanga, Dk. Paul Kisaka alisema tayari mkoa uko katika mikakati ya kuendeleza kupanda miti, ikiwa ni jitihada za kutunza mazingira.

"Hivi karibuni, tukiwa na maadhimisho ya Wiki ya Uvuvi, tulipanda mikoko, lengo ni kutunza mazingira ya bahari, lakini tumekuwa tunahamasisha na wananchi mmoja kuweza kushiriki katika kupanda miti kwenye maeneo yao," alisema Dk. Kisaka.

Ofisa Elimu ya Awali na Msingi Jiji la Tanga, Shomari Bane, alisema upandaji miti utafanyika katika shule sita za msingi wa jijini humo na kuwataka walimu na watendaji kusimamia ili mchakato huo ulete matokeo chanya.

"Upandaji miti ni sehemu ya uboreshaji mazingira kwa kuwa wanafunzi wataweza kupata maeneo ambayo yapo mazuri katika kujifunza," alisema Bane.

Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya Mwaka 1999 na Sheria ya Misitu, Sura 323, zimeweka utaratibu wa kisheria wa kudhibiti uharibifu wa mazingira hususan ukataji miti holela katika maeneo mbalimbali yakiwamo maeneo ya milima na miinuko.

Katika kukabiliana na uharibifu wa mazingira, Tanzania pia inatekeleza Ajenga ya Nishati Safi. Uharibifu wa mazingira nchini kwa mwaka ni wastani wa takriban hekta 400,000 zinazoharibiwa msituni kutokana na ukataji miti.



Wanachama wa Jumuiya ya Sikh (Singa Singa), wakichangia damu kwa ajili ya wahitaji mbalimbali, wakati wa hafla ya kumbukumbu ya kumuenzi Mtume wa Tisa "Guru Tegh Bahadur" jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Malori yanayoegeshwa barabarani yageuka kero

**Na Joseph Mwendapole**

MALORI yanayoegeshwa barabarani eneo la Saza Road, Kata ya Chang'ombe, Dar es Salaam yamegeuka kuwa kero kwa wananchi, wakiomba serikali kuchukua hatua kumaliza changamoto ya msongamano wa malori hayo.

Wananchi wamemweleza mwandishi kuwa malori hayo yamekuwa yanaegeshwa barabarani, hivyo kufunga barabara na kusababisha watumiaji wengine wa barabara kushindwa kupita.

Mmoja wa watumiaji wa barabara hiyo, Amir John alimwomba Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, kufika eneo hilo kuona hali halisi, akisisitiza "ni hatari iwapo janga la moto litatokea".

"Mtaa wa Saza Road na Mwakalinga, hii njia muda wote malori yameegeshwa barabarani, hakuna pa kupita kabisa na tunajiuliza iwapo itatokea dharura ya moto magari ya zimamoto yatapita wapi, viongozi wa mkoa na wilaya ya Temeke na hata kitaifa waje waone na kutatua kero hii.

"Waje waone hasa wakati wa mchana na jioni hali inakuwa mbaya sana, malori yameegeshwa barabarani jambo ambalo linasababisha njia inafunga kabisa, tunawaomba viongozi watembelee eneo hili waone hii shida ya hapa," alisema mtumiaji mwingine wa barabara hiyo, John Mwakitwange.

Mtumiaji mwingine wa barabara hiyo, Ali Mwamponda alisema hali hiyo imekuwa kwa muda mrefu. Imekuwa mbaya zaidi kwa wiki mbili sasa baada ya kipande cha barabara ya Mtaa wa Saza kufungwa kwa ajili ya ukarabati mdogo.

**"Ninashukuru kwa taarifa na nimeshamjulisha Meneja wa TARURA Wilaya ya Temeke atalifanyia kazi. Kwa sasa niko kwenye mkutano," alisema Mapunda.**

Alisema mkandarasi anayejenga kipande hicho amechimba na kufunga barabara hiyo inayopitisha malori kwa ajili ya kwenda viwandani kupeleka malighafi na kuchukua bidhaa mbalimbali baada ya uzalishaji.

"Foleni hapa ni maisha ya kawaida lakini hali mbaya unayoona hapa imesababishwa na kufungwa kwa kipande kifupi cha barabara Mtaa wa Saza, hivyo malori yaliyokuwa yanakwenda kule viwandani yanaegeshwa hapa barabarani," alisema.

"Tunaomba mamlaka zitusaidie kwa kweli maana mitaa yote miwili ya Saza na ule wa Mwakalinga inazibwa na malori yanayoegeshwa barabarani. Sasa watu wanaotaka kutoka kazini jioni unaweza kukaa hapa mpaka saa tano usiku maana hakuna njia. Asubuhi unakuja vizuri lakini jioni ni majanga makubwa sana," alilalama.

Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Sixtus Mapunda alipoelezwa kuhusu msongamano huo wa malori, alisema amemwagiza Meneja wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) kulifanyia kazi.

"Ninashukuru kwa taarifa na nimeshamjulisha Meneja wa TARURA Wilaya ya Temeke atalifanyia kazi. Kwa sasa niko kwenye mkutano," alisema Mapunda.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Wapandishwa kizimbani mashtaka dawa za kulevya

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

MKAZI wa Mtaa wa Mkomwa, jijini Dodoma, Suleiman Suleiman (52), maarufu Nyanda, na mwenzake wamefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Dodoma wakikabiliwa na mashtaka mawili ya kusafirisha dawa za kulevya aina ya Heroin zenye uzito wa gramu 392.49.

Akisoma maelezo ya shauri hilo namba 33719/2024 la uhujumu uchumi, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu wa Mahakama hiyo, Daniel Mpelembwa, Wakili wa Serikali Meshack Lwabonga, alimtaja mshtakiwa mwingine kuwa ni mkazi wa Airport Dodoma, Kimwaga Lazaro (37).

Alisema shtaka la kwanza linamkabili Suleiman peke yake. Anadaiwa kusafirisha dawa hizo. Novemba 7 mwaka huu maeneo ya Swaswa, jijini Dodoma, alikamatwa akisafirisha dawa aina ya Heroin zenye uzito wa gramu 323.

"Shtaka la pili linawakabili wote wawili Suleiman na Kimwaga ambapo siku hiyo ya Novemba 7, mwaka huu, eneo la Kinyali, maarufu Chako ni Chako, jijini Dodoma, walikamatwa na dawa aina ya Heroin zenye uzito wa gramu 69.46," alidai.

Alidai kuwa upelekezi wa shauri hilo haujakamilika na kuomba kupangiwa tarehe nyingine kwa ajili ya kutajwa.

Hata hivyo, baada ya kusomewa mashtaka hayo watuhumiwa hao hawakutakiwa kujibu chochote katika mahakama hiyo kwa kuwa haina uwezo wa kusikiliza kesi hiyo.

Hakimu Mpembelwa alisema mashtaka wanayoshtakiwa kwayo kwa hatua ya awali hayana dhamana na kesi imeahirishwa hadi Desemba 16, 2024 itapokuja kwa ajili ya kutajwa na washtakiwa wataendelea kukaa rumande.

# Z'bar kuunga mkono mradi wa USAID

**Na Getrude Mbago**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imeahidi kuendelea kuunga mkono Mradi wa USAID Kizazi Hodari unaolenga kusaidia kuboresha afya, ustawi na usalama wa watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu (OVC) na vijana walio katika jamii zinazokabiliwa na tatizo la Virusi vya Ukimwi (VVU) Zanzibar.

Kauli hiyo ilitolewa jana Zanzibar na Waziri wa Zanzibar Ofisi ya Rais - Mamlaka ya Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu (TAMISEMI & SD), Massoud Ali Mohammed, alipokutana na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Deloitte Africa Ruwayda Redfearn aliyefanya ziara Zanzibar kwa lengo la kupata ufahamu wa jinsi ya utekelezaji Mradi wa USAID Kizazi Hodari pamoja wapokeaji huduma za watu wanaoishi na kupokea dawa za kupunguza makali ya VVU (RoC).

Mradi wa USAID Kizazi Hodari Kanda ya Kusini (KHSZ) ni wa miaka mitano (Machi 2022 - Machi 2027), unafadhiliwa na Watu wa Marekani kupitia USAID na unatekelezwa na Deloitte Consulting Limited kwa kushirikiana na mashirika ya kiraia (AZAKi).

Waziri Massoud Ali Mohammed alisema Serikali ya Zanzibar inaelewa juhudi zinazofanywa na mradi wa USAID Kizazi Hodari katika kuboresha afya, ustawi na usalama wa watoto yatima na wanaoishi katika mazingira hatarishi (OVC) na vijana walio katika jamii yenye matatizo makubwa ya VVU Zanzibar.

"Miradi hii inakwenda mashinani na inawagusa walengwa moja kwa moja. Tunaelewa jinsi matatizo ya watoto wetu wanaoishi na VVU yanavyoenda na hasa pale ambapo wazazi wao wanapokuwa wamefariki dunia.

"Sisi serikali ya Zanzibar tunathamini juhudi hizo na tunaendelea kujitolea na tunatoa msaada wetu wote unaohitajika katika kufanikisha mafanikio ya mradi huu," alisema Waziri Massoud.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Deloitte Africa, Ruwayda Redfearn alipongeza Serikali ya Zanzibar kwa msaada wa ushirikiano ambao mradi wa USAID Kizazi Hodari imekuwa ikipata wakati wa kutekeleza mradi wa huu.

"Nimefurahishwa sana na ushirikiano wa serikali ambao tumekuwa tukipata wakati wa kutekeleza mradi huu. Tumekuwa tukifanya kazi na wizara mbalimbali za serikali na kila shughuli imekuwa ikiendelea vizuri," alisema.

Aliongeza kuwa amefurahishwa na kujifunza kuhusu jukumu la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kusaidia Mradi wa USAID Kizazi Hodari na mipango ya kuendeleza huduma hizo katika siku zijazo.

Mtendaji Mkuu wa Deloitte kwa Afrika Mashariki, Anne Muraya alisema kuwa mradi wa USAID Kizazi Hodari unalenga watoto na familia kwa lengo kuu la kuboresha afya, ustawi na usalama wa watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu na hatarishi wenye umri wa miaka 0-17 katika jumuiya zenye mizigo mikubwa pamoja na vipaumbele vinne muhimu vya huduma ambavyo ni afya, usalama, elimu na uthabiti.

Muraya aliongeza, "Katika mradi unaozingatia familia kama vile USAID Kizazi Hodari, wanawake wana jukumu muhimu kama watendaji wakuu katika muhtasari wa mradi na kubadilisha mazingira katika kuchangia lengo la kimataifa la 95-95-95 ambalo ni asilimia 95 ya watu wote wanaohisiwa kuwa na maambukizo wafahamu hali zao kiafya, asilimia 95 ya wanaoishi na maambukizi ya VVU kupokea tiba endelevu ya kurefusha maisha, na asilimia 95 ya watu wote wanaopata tiba ya kurefusha maisha kupata ukandamizaji wa virusi ifikapo 2030."


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya Kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania)**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya leseni ya kuzalisha umeme kutoka kwa Kampuni ya Gas Company (T) Limited. EWURA inakaribisha maoni au pingamizi kuhusiana na maombi hayo ya leseni. Taarifa za mwombaji pamoja na aina ya leseni iliyoombwa zimetolewa hapa chini:

| KIFUNGU | MAELEZO |
|---|---|
| Jina na anuani ya Mwombaji | Gas Company (T) Limited, S.L.P 714, Dar es Salaam. |
| Mahali ulipo Mtambo | Kiwanja namba 1, Kitalu A, Kisiwa cha Songosongo, Mkoa wa Lindi. |
| Taarifa za Wanahisa | Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania S.L.P 2774, Dar es Salaam, 100%. |
| Maelezo ya Mtambo na Matumizi | Kuzalisha umeme wa Megawati Kumi Nukta Saba (10.7) kwa kutumia gesi asili. Umeme utakaozalishwa utatumika kuendesha mitambo ya kuchakata gesi. |
| Aina na Muda wa Leseni | Leseni ya kuzalisha umeme kwa muda wa miaka mitano (5) |

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi kuhusu maombi haya awasilishe kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja (21) tangu siku ya kutolewa kwa tangazo hili. Nyaraka za maombi ya leseni zinaweza kuoneshwa baada ya maombi kwa maandishi.

**Imetolea na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**
**1 Desemba 2024**

182789

Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA , 41104 Tambukareli, S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 26 2329002 – 4 • Nukushi: +255 26 2329005 • Barua Pepe: info@ewura.go tz



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya Kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania)**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya leseni ya kuzalisha umeme kutoka kwa Kampuni ya "Gas Company (T) Limited". EWURA inakaribisha maoni au pingamizi kuhusiana na maombi hayo ya leseni. Taarifa za mwombaji pamoja na aina ya leseni iliyoombwa zimetolewa hapa chini:

| KIFUNGU | MAELEZO |
|---|---|
| Jina na anuani ya Mwombaji | Gas Company (T) Limited, S.L.P 714, Dar es Salaam. |
| Mahali ulipo Mtambo | Kiwanja namba 7, Kitalu A, Kata ya Madimba, Mkoa wa Mtwara |
| Taarifa za Wanahisa | Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania S.L.P 2774, Dar es Salaam, **100%.** |
| Maelezo ya Mtambo na Matumizi | Kuzalisha umeme wa Megawati Tatu (3) kutumia gesi asili. Umeme utakaozalishwa utatumika kuendesha mitambo ya kuchakata gesi. |
| Aina na Muda wa Leseni | Leseni ya kuzalisha umeme kwa muda wa miaka mitano (5) |

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi kuhusu maombi haya awasilishe kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja (21) tangu siku ya kutolewa kwa tangazo hili. Nyaraka za maombi ya leseni zinaweza kuoneshwa baada ya maombi kwa maandishi.

**Imetolea na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**
**1 Desemba 2024**

182789

Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA , 41104 Tambukareli, S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 26 2329002 – 4 • Nukushi: +255 26 2329005 • Barua Pepe: info@ewura.go tz



# Apendekeza kuanzishwa mahakama maalumu itakayosikiliza kesi za ukatili

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MWANAHARAKATI Aginatha Rutazaa, ameiomba serikali kuunda mahakama maalum itakayokuwa na jukumu la kushughulikia kesi pekee zinazohusu ukatili wa kijinsia.

Rutazaa, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la TUSONGE CDO, alisema kesi hizo kwa sasa zinashughulikiwa katika mahakama za kawaida na mara nyingi hazipati uzito wake wa kufanyiwa kazi kwa haraka, kwa ajili ya kusaidia waathirika waliofanyiwa matukio hayo.

Alikuwa akizungumzia jana siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia zilizoanza Novemba 25 na zikitarajiwa kufikia ukomo wake Desemba 10, mwaka huu.

"Tunajua kesi hizi zinashughulikiwa katika mahakama za kawaida na mara nyingi hazipati ule uzito wa kufanyiwa kazi kwa haraka kwa ajili ya kusaidia waathirika waliofanyiwa matukio haya.

"Kwa hiyo tunatamani sana kuishawishi na kuendelea kungana na wanaharakati wengine duniani kuomba serikali tukiihimiza tuweze kuwa na mahakama maalum itakayokuwa inashughulikia tu masuala ya ukatili wa kijinsia.

...Kwa wiki hii tunaungana na wenzetu wa dunia nzima kutokomeza ukatili wa kijinsia duniani na hususani Tanzania. Sisi kama taasisi ya kijamii iliyoko Kilimanjaro, Tusonge Community Development Organization, tunapenda pia kuwa sehemu ya hizi harakati za kupambana katika kutokomeza ukatili wa kijinsia."

Aidha, alisema TUSONGE ina maeneo machache ambayo wanapenda kukazia, ili pia kuweka msisitizo ukatili huo utokomee.

Alisema wanaomba serikali iendelee kuangalia kwa makini na kuweka sheria mahususi inayoshughulikia masuala au kesi za ukatili wa kijinsia ndani ya jamii.

Rutazaa alisema wanatamani pia mifumo ya kisheria inayohusika na utatuzi iangalie suala zima la ukatili wa kijinsia.

"Tuiombe jamii iache kutumia ile mifumo ya kijamii au ile ya mila ambayo inazidi kuendelea kukuza usawa na kupinga ukatili wa kijinsia ndani ya jamii. Kwa mfano kukaa kwenye ukoo, kujadiliana wazazi, ndugu, walezi mnaacha waathirika waliofanyiwa tukio lile bila kujua mustakabali wa haki zake zikoje.

"Kwenye jamii mfano ya Mkoa wa Kilimanjaro, kuna suala zima la kutumia masale, lile jani la amani ambalo pia wazazi wanakuja nalo kama alama ya kuomba msamaha baada ya mtu kufanyiwa tukio kubwa na lenye majeraha makubwa katika maisha yake.

Zaidi aliongeza: "Kwa hiyo tunatamani kwamba jamii nayo ichukue jukumu la kutumia ile mifumo sahihi ya kuripoti matukio ya ukatili ambayo ni mifumo ya kisheria, ili sheria zile zilizowekwa zichukue hatua na zichukue mkondo wake.

Alisema eneo lingine ni viongozi waliochaguliwa wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji, waangalie kwa kina kwa sababu matukio haya yanatokea ndani ya mitaa na ndani ya vijiji na vitongoji.



Mganga Mkuu wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Dk. Fani Mussa (kulia), akijadiliana jambo na watumishi wa Idara ya Afya wa wilaya hiyo, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani, yaliyofanyika kiwilaya katika kijiji cha Kigombe, juzi usiku. Kushoto ni Mratibu wa UKIMWI wa wilaya hiyo, Mohamed Bakari. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# ACT-Wazalendo, CUF walaani matukio utekaji

**Na Oscar Assenga,** TANGA

VIONGOZI wa vyama vya siasa vya ACT -Wazalendo na Chama cha Wananchi (CUF) Mkoa wa Tanga vimelaani vitendo vya utekaji vinavyoendelea, huku wakilitaka Jeshi la Polisi kuhakikisha wanavikomesha ili visilitie doa taifa.

Hatua ya viongozi inatokana na Kiongozi wa Ngome ya Vijana ya ACT-Wazalendo, Abdul Nondo kuchukuliwa na watu wasiojulikana katika eneo la Stendi ya Magufuli Mbezi Louis Dar es Salaam Desemba 1, mwaka huu wakati akitokea Kigoma.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na Nipashe jana viongozi hao walisema kwamba hilo siyo jambo jema kwa sababu linawapa hofu wananchi na wanasiasa hasa wakati wanapoelekea kwenye Uchaguzi Mkuu mwakani.

Katibu wa ACT-Wazalendo Mkoa wa Tanga, Mussa Kassim Mbega, alisema jukumu la Jeshi la Polisi ni kulinda raia na mali zao na inapofikia mahali hawana uhakika na mali zao inapelekea wananchi kuwa na taharuki kwamba kweli wapo huru.

Alisema kwamba matukio hayo sio tishio kwa wanasiasa bali na wananchi na hilo limekuwa ni janga la kitaifa na kunahitajika kuwapo kwa mjadala wa kitaifa, ili mambo ya aina hiyo yaweza kwisha maana yamekuwa yakijitokeza mara kwa mara.

"Mara ya mwisho Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, wakati akiwa kwenye msiba wa kada wa Chadema Ally Kibao alisema wahusika watapatikana lakini mpaka sasa bado, hivyo tunaomba Jeshi la Polisi vikiwemo vyombo vya ulinzi kuhakikisha mambo kama hayo hayajitokezi tena kwa jamii," alisema.

Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF) Wilaya ya Tanga, Mussa Mbaruku alisema kwamba mambo ya kutekekana yamekuwa yakiitia doa serikali kwa maana wanaotekwa wanaambiwa kuna tume imeundwa lakini hakuna chochote kinachoendelea.

"Kwa maana tulisema kuna kamati imeundwa lakini mambo ya kutekana yamekuwa ni kama jambo la kawaida Tanzania kwani mambo hayo tuliyasikia nchi za jirani na yasipochukuliwa hatua yatakwenda mbali sana," alisema.

Alisema itafikia hatua mtu akifumaniwa na mke wa mtu atatekwa huku akitaka wanaopatikana na hatia ya utekaji wachukuliwa hatua kali za kisheria ili kudhibiti vitendo vya namna hiyo hapa nchini.

# TEHAMA yasaidia usikilizaji, utoaji hukumu kwa wakati

**Na Allan Isack,** ARUSHA

RAIS wa Chama cha Majaji na Mahakimu Tanzania (JMAT), John Kahyoza, amesema mahakama za Tanzania zimepiga hatua katika usikilizaji wa kesi na utoaji wa hukumu kwa wakati, kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Kahyoza ambaye ni Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Manyara, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na maandalizi ya mkutano wa 21 wa Chama cha Mahakimu na Majaji wa Afrika Mashariki (EAMJA), unaofanyika jijini Arusha kuanzia Desemba 2 hadi 7 mwaka huu.

Ufunguzi wa mkutano huo utafunguliwa leo (kesho), na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ambaye atakuwa mgeni rasmi.

Alisema TEHAMA imesaidia kurahisisha ufunguaji wa kesi kwa njia ya mtandao, kuendesha mashauri kwa njia ya mtandao, kupunguza muda wa mashauri kuwa mahakamani na kupunguza viashiria vya rushwa.


Kadhalika, alisema mfumo huo umewasaidia majaji na mahakimu kutoa hukumu kwa haraka na kwa wakati ukilingalisha na ilivyokuwa huko nyuma.

Vilevile, alisema kutokana na maboresho yaliyofanyika katika mahakama za Tanzania nchi imefaidika kwa kuwa migogoro au kesi zinatatuliwa kwa wakati na wananchi wanakwenda kuendelea na shughuliza uzalishaji mali.

"Hatuwezi kuzuia migogoro isitokee ila inapotokea inatatuliwa kwa haraka ili wananchi wakaendelee na shughuli za uzalishaji mali kwa ajili ya kukuza uchumi wa nchi na familia zao," alisema Jaji Kahyoza.

Alisema zaidi ya washiriki 392 watashiriki katika kongamano na mkutano mkuu na tayari wageni wameshawasili jijini Arusha na maandalizi yamekamilika.

Alisema washiriki wa mkutano huo wanatoka katika nchi za Tanzania, Uganda, Kenya, Rwanda, Burundi, Sudani ya Kusini na Zanzibar.





# Matababibu tarajali walia ubovu wa miundombinu chuoni

Na Alex Sayi, MASWA

WANAFUNZI wa Chuo cha Maofisa Tabibu, kilichoko wilayani Maswa mkoani Simiyu wameiomba serikali kuwasaidia kuboresha miundombinu ya chuo hicho.

Ombi hilo limetolewa na wanachuo hao mbele ya Naibu Waziri wa Afya wakati wa maadhimisho ya miaka 50 ya chuo hicho, yaliyokwenda sambamba na mahafali ya 48 ya chuo hicho.

Rais wa Serikali ya Wanafunzi wa chuo hicho, Simba Gulala, alisema miundombinu ya chuo hicho kilichoanzishwa mwaka 1974 ni chakavu hasa madarasa, mabweni huku wakiwa na uhaba wa vifaa vya kujifunzia.

"Tunaiomba serikali ituboreshee miundombinu ya chuo ili iweze kuendana na wakati uliopo kwani kwa sasa miundombinu ya chuo hiki ni mibovu," alisema Gulala.

Mkuu wa chuo hicho, Dk.Hangwa Enos licha ya kukiri ubovu wa miundombinu chuoni hapo alisema kwa sasa wanakabiliwa na uhaba wa watumishi, uhaba wa vifaa vya kujifunzia ikiwamo kompyuta na midoli.

Alisema ndani ya miaka 50 chuo hicho kimetoa wahitimu 2,255 kwa fani ya utabibu pamoja na wahitimu 84 wa mwaka huu.

"Chuo kina malengo ya kuanzisha programu tatu zitakazosaidia kupandisha udahili wa wanafunzi kutoka 270 hadi 960, hivyo ili kufikia lengo hili tunaiomba wizara kusaidia kupatikana kwa fedha kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu na kuharakishwa kwa ujenzi wa jengo la kitaluma," alisema Dk.Hangwa.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel alisema serikali tayari imeona hali ya ubovu wa miundombinu chuoni hapo na kuwa imetenga Sh.bilioni 2.9 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kisasa, itakayosaidia kuboresha hali ya usomaji kwa wanfunzi hao.

Alisema maboresho hayo yanatarajiwa kuanza hivi karibuni na ujenzi wake utakamilika Septemba, 2025 na kukifanya chuo hicho kutoa elimu kwa vitendo na kuzalisha wahitimu wenye ufanisi kazini.




Mafundi wakiendelea kuziba viraka kwa kutumia zege katika Barabara ya Lumelezi, ambayo ni lango la kuingilia kituo cha mabasi ya Kahama, mkoani Shinyanga, jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Viongozi S/mitaa wakumbushwa wajibu wao

Na Waandishi Wetu

VIONGOZI wa Serikali za Mitaa wamepewa angalizo juu ya usimamizi wa shughuli za maendeleo ikiwa ni pamoja na kuwasomea wananchi mapato na matumizi na udhibiti vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Wito huo umetolewa na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha, wakati wa uapisho wa viongozi hao, huku akiwataka kufanya shughuli zao kwa kuzingatia miongozo na taratibu.

Kadhalika, aliwataka viongozi hao kwenda mitaani na kufanya mikutano ya kijiji, kujadili shughuli za maendeleo, pamoja na kusomea wananchi mapato na matumizi, siyo kuwachangisha wananchi michango bila kuwapa taarifa.

Pia, aliwataka kwenda kusimamia amani katika maeneo yao, kuwatambua watu, kuhimiza shughuli za maendeleo, kusimamia miradi, kutatua migogoro ya ardhi, kutunza mazingira, usafi, kupanda miti, kuwasisitiza wananchi wafanye kazi, pamoja na kuchangia chakula shuleni.

Akizungumza katika hafla ya kuchangia fedha na vifaa kwa watu wasioona iliyoandaliwa na wananchi katika eneo la uchimbaji madini la Nyamongo, Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Edward Gowele, aliagiza viongozi wote ngazi za vijiji na mitaa kuweka maslahi ya watu wenye ulemavu mbele wakati wakitoa huduma katika maeneo yao.

Alisema kundi hilo wamekuwa wakipata changamoto kufikia huduma za jamii zikiwamo afya na elimu kutokana na upungufu wa vifaa na miundombinu isiyo rafiki kwao.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, Rose Manumba, aliwaagiza viongozi hao kuhakikisha wanakuwa mstari wa mbele kupambana dhidi ya vitendo vya ukatili katika maeneo yao.

Manumba alisema vitendo vya ukatili wa kijinsia vinavyotokana na mila na desturi potofu zinazosababisha mabinti wengi vijijini kukatisha ndoto zao za kielimu kwa kuozeshwa kwa tamaa za wazazi za kutaka mali.

"Hakikisheni hakuna vitendo vya ukatili vinavyoweza kutokea kwenye maeneo yenu na hamtakiwi kuwa sehemu ya vitendo hivyo kwa kigezo cha kujipatia fedha kwani nafasi mlizonazo siyo sehemu ya chanzo cha mapato ya familia zao," alisema Manumba.

Vilevile, aliwataka kutokuwa chanzo cha migogoro ya ardhi kwa kujihusisha na uuzaji wa viwanja kwa zaidi ya wananchi wawili kwa tamaa ya kutaka fedha, kwani ofisi za serikali za vijiji na vitongoji siyo chanzo cha mapato ya halmashauri wala familia.

Ofisa Rasilimali Watu na Utawala wa Halmashauri ya Msalala, Merry Nziku aliwataka viongozi hao kufanyakazi kwa kuzingatia viapo walivyoapa mbele ya hakimu, siyo kuwa sehemu ya kutoa siri za wananchi hadharani na kuwa chanzo cha migogoro.

**Imeandaliwa na Shaban Njia (Kahama), Marco Maduhu (Shinyanga), Ambrose Wantaigwa (Tarime).**

## Bashungwa aagiza umakini ujenzi madaraja korofi

Na Marco Maduhu, USHETU

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, amemwagiza Meneja Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Shinyanga Samweli Mwambungu, kuwasimamia vizuri makandarasi ambao wanajenga madaraja katika Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama kuhakikisha yanakuwa ubora na kuendana na thamani ya fedha.

Alitoa agizo hilo juzi wakati akikagua maendeleo ya ujenzi wa madaraja matatu, ambayo yanajengwa katika halmashauri hiyo kupitia mfuko wa kurudisha barabara na madaraja korofi ambayo yaliharibiwa na mvua za Eli-Nino na Kimbunga Hidaya nchini.

Alisema serikali imetoa Sh. bilioni 868 ili kukarabati miundombinu hiyo na kuwa katika Halmashauri ya Ushetu zimetolewa Sh.bilioni 13.5 kujenga madaraja matatu.

Aidha, alimwagiza pia meneja huyo kuhakikisha anapeleka mkandarasi kwenye ujenzi wa daraja ambalo linaunganisha Ushetu na Mkoa wa Geita ili ujenzi uanze mara moja.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha, alisema ujenzi wa madaraja hayo ni mkombozi kwa wananchi na kwamba katika Halmashauri ya Ushetu wananchi wengi shughuli zao ni kilimo cha tumbaku.

Alisema ujenzi wa madaraja hayo yatakuwa yakiwasaidia katika shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwamo kusafirisha mazao.

Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani, alisema kiu kubwa ya wananchi wa jimbo hilo ni kuwa na madaraja, lakini sasa hivi tatizo hilo serikali inakwenda kulitatua.

Meneja TANROADS, Mkoa wa Geita, Samweli Mwambungu, awali akitoa taarifa ya ujenzi wa madaraja hayo alisema mikataba ya ujenzi wake ni miezi 12.

Aliyataja madaraja hayo kuwa ni Daraja la Ubagwe lenye thamani ya Sh. bilioni 4.1, Daraja la Kasenga Sh.bilioni 5.1 na Daraja la Ng'wande Sh.bilioni 4.1 na kwamba jumla ya gharama zote za ujenzi wa madaraja hayo ni Sh.bilioni 13.5.

Mmoja wa makandarasi ambao wanatekeleza ujenzi wa Daraja la Ubagwe, Godfrey Mbande, alisema ujenzi huo watautekeleza ndani ya muda uliopangwa.



Ukurasa 12

**Tabianchi inavyoweka maisha uchumi rehani**



Ukurasa 13

Kuepuka msongo, shida afya akili TANCDA yaja na darasa kujinasua

Nipashe

# TESA

Jumanne Desemba 3, 2024

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

**SIKU 16 UKATILI...**

**Wazazi wakagueni watoto wenu acheni kuwaachia babu, bibi ulezi**

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

SIKU 16 VS UKATILI KIJINSIA

# Watetezi wanapoonya unyanyapaa watumishi wa ndani WAVIU ukomeshwe, walindwe

JUMAPILI Desemba mosi, iliyokuwa Siku ya UKIMWI Duniani, zimesikika ripoti na kazi mbalimbali zikizungumzia hali ya maambukizi, mafanikio, changamoto bila kusahau ukweli kuwa mambo ni mabayá zaidi kwa waathirika wanawake na watoto.

Mkoani Mara Shirika la Haki Sawa kwa Wote, linalotetea ustawi wa wafanyakazi wa nyumbani, linasema wasichana watumishi wa ndani walioathirika na VVU wanapogundulika na waajiri wao baadhi wananyanyapaliwa na kuumizwa zaidi.

Mkurugenzi wa Haki Sawa, Angelina Nyamusika, akizungumzia harakati za siku 16 za kupinga ukatili, anasema wamejikita kwenye VVU, kuwasaidia mabinti wanaoishi na maradhi hayo.

Kwa kushirikiana na viongozi wa serikali, waajiri na asasi za kiraia wanawahamasisha wafanyakazi hao kupima VVU kujua hali zao, kujitibu na kuchukua tahadhari.

Anasema wanalenga kuwapunguzia kunyanyapaliwa endapo watagunduliwa kuwa wanaishi na VVU na pia kuwasaidia kufikia huduma za tiba kinga zinazogharamiwa na serikali.

"Tunataka watumishi wa ndani wenye VVU wajitambue, pia waajiri na wazazi au walezi wafahamu na kuwasaidia kupata huduma. Tunalenga kuongeza ustawi wa maisha yao na pia kupunguza maambukizi mapya." Anasema Angelina.

"Kwa kuanza tulilenga kuwafikia wasichana watumishi wa majumbani 25 hapa wilayani Musoma, baada ya kuomba kibali cha halmashauri tukishirikiana na viongozi wa serikali za mitaa tukawatembelea na kuanza utekelezaji.

Aidha, tukawaelimisha waajiri na kuwashawishi wasichana hao kukubali kuchunguzwa afya na kati yao 10 walikubali na wengine 15 hawakuwa tayari.

Anaeleza kuwa wamewashirikisha wazazi, walezi pamoja na waajiri wa wasichana hao kabla ya kuwapima na kwamba sheria inaelekeza kuwa endapo binti hajafikia miaka 18 ni lazima mzazi au mlezi atoe ridhaa ya kumpima mtoto VVU. Anasema kazi ya kupinga ukatili dhidi ya watumishi wa ndani wanaoishi na VVU imefanyika maeneo ya Mlimani, Mshikamano na Nyakato katika Halmashauri ya Musoma.

"Kuwapima na kuwatambua na kuhamasisha mitandao mingine kufanya hivyo kunalenga iwe chachu ya kupunguza unyanyapaa mitaani na nyumbani kwa hiyo tunachotaka ni heshima na kuwathamini wenzetu.

Umma utambue kuwa kuishi na VVU hakuondoi haki ya kulipwa mshahara kisheria, kufanyakazi na kupata riziki yako na kwamba hata kama ni MVIU bado ni binadamu na unastahili haki sawa," anasema Angelina.

Anaongeza kuwa wapo baadhi ya waajiri au jamaa zao wanaowabaka watumishi wa ndani na kuwaambukiza VVU, lakini wakigundulika wana maambukizo wasichana hao hunyanyapaliwa, kadhalika wanafukuzwa na pengine hata bila kuwalipa mishahara.

Pia, kuna wale wanaokataa kuwalipa watumishi wa ndani Shilingi 60,000 kwa mwezi ambacho ni kiwango cha mishahara yao kisheria. Tena kuna wengine waolimbikiza mishahara hiyo na kesi kama hizo zinakuja kwenye ofisi za Haki Sawa kwa Wote.




Mkurugenzi Mtendaji, Angelina Nyamhanga akishikilia bango kutetea haki za watumishi wa ndani. **PICHA: HAKISAWA**

Anasema wamewajengea uwezo wa kukabiliana na unyanyapaa. Wanataka kuweka tabasamu kwenye nyuso za wasichana hao hata kama wanaoishi na VVU wajue kuwa wana haki, wanawajali na wasijinyanyapae.

Godwin Charles ni Mratibu wa Haki Sawa kwa Wote mkoani Mara, akizungumzia jitihada hizo, anasema shirika hilo lenye wanachama zaidi ya 61, wanatetea haki za watumishi hao kupunguza unyanyapaa na ukatili dhidi ya Wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI (WAVIU).

Anaeleza kuwa walipokuwa wanafanya kampeni za kuwachunguza afya, waliwashirikisha wazazi na walezi wa mabinti, waajiri na wao wenyewe, lakini idadi kubwa haikuonyesha ushirikiano.

Anasema baadhi ya walezi na wazazi walikataa wasichana kuchunguzwa wakisema waachwe na hivyo hawakuwapima.

Anaeleza kuwa lengo ni pale wanapowagundua kuwa ni WAVIU wataalamu wawape ushauri, kisha waajiri, wazazi au walezi wafahamu kuhusu hali zao na kuwashauri wasiwanyanyapae na hata WAVIU wasijinyanyapae.

"Tunawafundisha njia za kuwa salama zaidi, hasa kwenda hospitalini, kujiandikisha na kuanza kutumia tiba kinga au ARV mara moja," anasema Charles.

Wanalolenga ni kuwaelimisha ili wajifahamu na kujikubali watumie tiba kinga na kujiepusha na kuwaambukiza wengine na kuongezewe virusi zaidi.

Charles anasema wakifahamu kuhusu hali zao kuwa wanaishi na maambukizi ya VVU watatumia tiba na pia waajiri watatengeneza utaratibu bora zaidi wa kuwahudumia na kuwawezesha kufanya majukumu yao au maamuzi mengine lakini yanayoheshimu na kuzingatia haki za binadamu.

Anakumbusha kuwa dunia ya leo mtu anaweza kupata chochote anachotaka bila kujali hali yoyote aliyo nayo hata kama anaishi na VVU.

Aidha, nawahimiza wanaoishi bila VVU kuwaheshimu na kuwathamini WAVIU kwa kuwa kila binadamu anastahili kuheshimiwa na kuthaminiwa utu

ELIMU

NA RAHMA SULEIMAN, ZANZIBAR

# Tabianchi inavyoweka maisha, uchumi rehani

• Maji bahari yazingira makazi, mashamba

MABADILIKO ya tabianchi ni tishio visiwani Zanzibar, kutokana na athari za moja kwa moja katika maisha ya wananchi, ambazo ni kuvuruga mwenendo wa maisha hususan wananchi wanaoishi katika ukanda wa pwani.

Miongoni mwa athari hizo ni maeneo mengi ya kilimo na makazi ya watu kuvamiwa na maji ya bahari yenye chumvi, kudhoofisha uchumi kwa kuharibu mavuno, kusababisha wananchi kuyumba kiuchumi na kiafya.

Kisiwa cha Uzi Ng'ambwa chenye wakazi 4,233 ni miongoni mwa maeneo 148 ya Zanzibar yalioathirika na mabadiliko ya tabianchi ikiwamo maji ya bahari kuzingira mashamba ya wakulima.

Utafiti wa athari za mabadiliko ya tabianchi kwa uchumi wa Zanzibar unabaini kuwa Zanzibar inakabiliwa na ongezeko la kiwango cha joto, kubadilika kwa majira ya mvua, kuongezeka upepo mkali wakati wa kusi na kaskazi, ongezeko la kina cha bahari, mawimbi yake na kuongezeka kwa matukio ya maafa, yote yakihusishwa na mabadiliko ya hali ya hewa.

Aidha, utafiti huo ulibaini kuwa karibu sekta zote kuu za uchumi wa Zanzibar zinaathiriwa na mabadiliko ya tabianchi na kuainisha kuwa Zanzibar ina maeneo 148 Unguja 25, Pemba 123 ambayo yameathirika kwa kuvamiwa na maji ya bahari wakati kilimo, uvuvi, utalii, maji, makazi na miundombinu ni sekta zinazoathirika zaidi.



Asha Ramadhan Bakari, mkulima kisiwani Uzi akiwa shambani na sasa analima kilimo mseto kukabili athari za mabadiliko ya tabianchi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

**KISIWA CHA UZI**

Riziki Shehe Yussuf, mkazi wa Uzi mkoa wa Kusini Unguja, anasema shamba lake analolima lenye ukubwa wa kilomita 120 limevamiwa na maji ya bahari na hakuna mazao yanayopatikana katika eneo hilo.

Anasema awali kabla ya maji ya bahari kuvamia eneo hilo, alilima mazao mihogo, mbaazi, mahindi na mazao mengine na akipata mavuno mengi lakini kwa sasa hakuna kinachopatikana.

Anaongeza kuwa kilimo hicho kilimsaidia kupata chakula kwa ajili ya familia yake na kupata fedha ya kujikimu kimaisha baada ya mauzo.

"Nilikuwa navuna muhogo mzuri, mtamu na mlaini nikiufikisha sokoni unagombaniwa maarufu mwari lakini hivi sasa haustawi maji ya bahari yamevamia mwaka huu. Ni miaka nane nalima sijapata kuona maji ya bahari kupanda juu kama ilivyo sasa," anasema.

Aidha, kilimo hicho kimeanza kuharibika kidogo kidogo ambapo muhogo alikuwa akivuna huwa mbovu bila ya kujua tatizo lililopelekea zao hilo kuharibika.

"Hivi sasa eneo hilo la kilimo nimeliacha maana hata ukilima huna unachokipata, na maisha yangu yamekuwa magumu maana wakati wa mavuno nilikuwa silali na njaa," anasema.

Sekta ya kilimo inatajwa kuajiri takribani asilimia 35 ya Wazanzibari huku zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wakitegemea sekta hiyo kujikimu kimaisha.

Kwa mujibu wa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo sekta hiyo inayojumuisha mazao, mifugo na maliasili za misitu ni tegemeo kwa uchumi wa Zanzibar na inachangia moja kwa moja kwa wananchi kujikimu kimaisha.

Asha Ramadhan Bakari, mkulima kiongozi kisiwa cha Uzi ambacho jografia yake inaonyesha kuwa kimezungukwa na bahari, anaungana na Riziki akisema mabadiliko ya tabianchi yameathiri kisiwa hicho kwa sababu kimekabiliwa na ukame na mvua zimekimbia na kukwamisha kilimo.

"Jua ni kali na kilimo kimekuwa kigumu kwa sababu mvua hakuna na mara zote mazao yanahitaji maji ili kukua na kupata mavuno mengi," anasema.

Anaongeza kuwa hata eneo ambalo maji ya bahari hayafiki, muhogo umeathirika na muhogo anaovuna haufai kuliwa kwa sababu una rangi ya njano na ladha yake siyo nzuri ni uchachu kama iliyowekwa ndimu.

Sheha wa Uzi Othman Mwinyi Haji, anasema kuna changamoto ya maji ya chumvi kutoka baharini kuingia kwenye mazao kutokana na watu kukata misitu ya mikoko.

Anasema kipindi cha nyuma maji ya bahari yalikuwa yakipanda angalau mara moja kwa mwaka lakini kwa sasa yanaingia mara kwa mara kutokana na uharibifu wa mazingira.

Miaka 20 iliyopita kisiwa cha Uzi kilikuwa na uoto wa asili na mandhari mazuri ya kimazingira lakini kwa sasa ni ukame kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi zilizotokana na uharibifu wa mazingira na kupelekea maji wa bahari kuvamia mashamba, anasema.

Aidha, miaka hiyo hata kina cha maji ya chumvi kilikuwa mbali lakini sasa ukichimba chini ya ardhi unakutana na maji ya chumvi jambo ambalo ni hatari kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Anasema mikakati ya pamoja inahitajika katika kukinusuru kisiwa hicho kisifunikwe na maji ya bahari, na miongoni mwa mikakati hiyo ni kupanda mikoko kwa wingi ambayo ndiyo mwarubaini wa kuzuia maji ya bahari kufika mashambani.

**WADAU WA MAENDELEO**

Ofisa teknolojia ya uzalishaji katika mradi wa Zanzibar Women Leadership in Adaptation (Zan Adapt), Shabani Peter, anasema kupitia mradi huo wanalenga kuwafikia wakulima 4,000 wakiwamo wa kisiwa cha Uzi kati ya hao asilimia 80 ni wanawake ili kuwapa elimu na mbinu za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ikiwamo kupanda miti.

Mradi huo unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Shirika la Kimataifa la Misitu (CFI) Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA Zanzibar), Jumuiya ya Misitu Pemba (CFP), wakiwezeshwa na Shirika la Global Affairs la Canada.

Peter anasema mradi huo zaidi unalenga wanawake kwa sababu ndiyo waathirika wakuu wa mabadiliko ya tabianchi, wakitambua namna ya kukabiliana nayo na wakiwa na vipato itasaidia kukuza uchumi na kuhifadhi mazingira.

Anasema lazima wawafundishe wakulima mbinu bora za kuzingatia mabadiliko ya hali ya hewa, kuhifadhi udongo na kuhifadhi unyevu unyevu.

Anasema miongoni mwa mbinu hizo ni kuhamasisha kilimo mseto ambacho kinaendana na mabadiliko ya tabianchi na kinachangia kupatikana mvua lakini pia ni kupanda miti ya mikoko ambayo inahimili mmong'onyoko wa fukwe na maji ya mahabari kupanda juu na kufikia makazi na mashamba.

**IDARA YA MISITU**

Mwatima Abdallah Khamis Ofisa Misitu Jamii kutoka idara ya misitu, anasema shughuli za kibinadamu ni sehemu kubwa inayochangia uharibifu wa mazingira hali ya ambayo inapelekea maji ya bahari kuvamia maeneo ya kilimo na hata makazi.

Anasema juhudi zinazofanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa mazingira kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kuhifadhi na kutunza mazingira ikiwamo upandaji wa miti kwa sababu miti huchangia kuleta mvua na kupunguza ukame.

Juhudi kubwa zinahitajika na ushirikiano wa pamoja ili kunusuru hali hiyo isiendelee kwa sababu inaathiri hata mipango ya serikali kuwaletea wananchi maendeleo ikiwamo utekelezaji wa sera ya uchumi wa buluu.

**KUTUNZA UDONGO**

Waziri wa Kilimo, Maliasili, Umwagiliaji na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, anasema udongo ni muhimili mkubwa kwenye kilimo cha kujikimu na kuchangia pato la taifa hivyo ni vyema utunzwe na kuhifadhiwa.

Zanzibar ina uchache wa ardhi kwa maeneo ya uzalishaji na kila mtu anahitaji kujikimu kimaisha kwa kilimo ndiyo maana serikali na washirika wa maendeleo ilifanya uchunguzi wa afya ya udongo Unguja na Pemba kubaini mapungufu ya wakulima ambayo ni fursa kwao ya uzalishaji, anasema.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar (ZARI), Dk. Mohamed Dhamir Kombo, anasema mwaka jana walifanya makubaliano ya mashirikiano na World Vegetable Center kufanya kazi kuongeza uzalishaji wa mazao.

ELIMU
NA GAUDENSIA MNGUMI

# Kuepuka msongo, shida afya akili TANCDA yaja na darasa kujinasua

AFYA ya akili ni jambo muhimu kwa ustawi wa binadamu kwa kila hali ila, hupuuzwa mara nyingi au ni tatizo lisilopewa kipaumbele na familia hata jamii kubwa.

Mpaka sasa inatokea kusiwe na msaada wala tiba, kuendeleza unyanyapaa dhidi ya wenye shida ya afya ya akili na wapo watu wanaoamini kuwa wenye shida hizo wamerogwa, ni mkosi au wameadhibiwa kutokana na matendo yao ya kihalifu.

Sababu mojawapo ya changamoto ya afya ya akili ni msongo wakati mwingine huitwa msongo wa mawazo. Wataalamu wa Shirikisho la Vyama vya Magonjwa yasiyoambukiza Tanzania (TANCDA), wanasema msongo ni hali inayojitokeza pale unapoona uwezo, maarifa au ujuzi hauendani na jambo lililo mbele yako.

Wanasema katika mazungumzo na machapisho waliyotoa wakati walipotembelea vyombo vya habari vya IPP Mikocheni Dar es Salaam na kuzungumza na wafanyakazi na kuwapima kisukari.

Wanaohudumiwa ni pamoja na wafanyakazi wa ITV, Radio One, East Televisheni, magazeti ya Nipashe na The Guardian na kuwapima uzito, sukari na kuwapa ushauri wa kiafya.

Wataalamu hao wanasema msongo unaweza kujitokeza pale malengo uliyojiwekea yasipotimia, au kufikiri hayatafanikiwa.

Kitabu cha Mtindo wa Maisha na Magonjwa yasiyoambukiza: Dalili, Athari na Kinga, kinachoandaliwa na TANCDA, kinaeleza kuwa msongo kwa kiwango fulani hufanikisha kuboresha utendaji kazi ila unapozidi unaathiri afya.

Wanakumbusha kuwa msongo husaidia mwili kupambana na hatari kwa kukimbia au kupambana, lakini ukiendelea kwa muda mrefu huongeza uwezekano wa kupata kisukari, shinikizo la damu, maradhi ya moyo, mishipa ya fahamu na fahamu, saratani na kuathiri mfumo wa kinga mwili.

Vyanzo vikuu vya msongo vinatajwa kuwa ni pamoja na mabadiliko ya kimaisha mfano kufiwa, kuugua, kuuguliwa, wasiwasi au mfadhaiko wa mambo ambayo yanaleta hofu licha ya kwamba hayajulikani. Kingine ni muda unaobakia kutimiza lengo au kufanya kitu, kukosa mpangilio na uchovu wa mwili.


Michezo na mazoezi huimarisha afya ya akili. **PICHA: MTANDAO**

### DALILI ZA MSONGO

Unadhihirika kwenye kuumwa kichwa, kukosa usingizi, hamu ya kula, kutokuwa na morali ya kufanya chochote au kutokufurahia kazi.

Nyingine kwa mujibu wa TANCDA ni uchovu wa mwili na akili, mabadiliko ya kihisia kama kukasirika kwa kitu kidogo, kupungua umakini au usahaulifu mara zote, kufanya makosa madogo madogo na kuwa na mawazo hasi zaidi wakati wote.

Dalili kama ulevi kupindukia, kutumia dawa za kulevya na tumbaku ni mojawapo ya mambo yanayoashiria kuwapo msongo wa mawazo. Ni vizuri kuwa na malengo lakini malengo yasiwe hayaendani na uwezo na iposhindikana kuyatimiza inakuwa vigumu kukubali ukweli.

### KUKABILI MSONGO

Unapopitia msongo wataalamu hao wanakushauri kuwa uwe na matumaini kwa kila tatizo, shida au changamoto unayopitia.

Fanya mambo yaliyo kwenye uwezo wako malengo au madhumuni yako kimwili, kiafya na kiroho kulingana vipaji ulivyo navyo ukizingatia jukumu lako, wanaongeza.

Kadhalika wanasisitiza kuwa na matumaini kuwa utafanikiwa kwa kila unachoamua, tena usipange kushindwa wala kukwama, kadhalika jijengee tabia ya kujitegemea kwa kujimudu mwenyewe na kujiendeleza kwa maeneo mbalimbali. Wanasema ni vyema kujenga umahiri wa kusimamia na kutumia muda ipasavyo na kupanga vipaumbele ili uwe na imani na uwezo wako wa kudhibiti mazingira yako.

Wanashauri pia kuwa makini na jambo moja kwa wakati mmoja. Pia kujifunza kukubali kuwa huwezi kushindwa kila kitu na uwe tayari kusema 'hapana', zinapokuja fikira mbovu. Wanasema ni vyema kugawa majukumu na kuomba msaada unapokwama au unapouhitaji.

Kuwa na tabia chanya na epuka kupima thamani yako mwenyewe kwa kujilinganisha na watu wengine, ni jambo jingine linalotajwa. Wanashauri kushikamana na kuwa na mawasiliano na wengine, kuwa rahisi na tayari kukubaliana na wengine, pia shirikisha wengine maisha kwani kuna changamoto hasi na chanya ambazo lazima kupitia.

Kushirikisha mtu unayemwamini changamoto na shida au kuzungumza na mtaalamu wa afya ya akili yanayokusibu kunapunguza athari na kutoa fursa ya kukabili tatizo au kuwa na uhimilivu wa kuendana nalo, wanasema wataalamu hao.

Aidha, TANCDA inashauri kuwa na muda wa kufurahia muziki, kucheka na kushiriki michezo, sherehe, tamasha, burudani na mambo ya kiroho.

> Pia wataalamu wanashauri kujenga tabia ya kushukuru kwa kila jambo, ulichonacho na kuweka orodha ya mambo unayoshukuru.

Shirikisho hilo linashauri pia kutumia muda kutembelea mazingira ya asili mfano misitu, wanyama, bahari, mito na kuangalia nyota angani kwa muda mfupi kama huna wa kutosha ili kuipa nguvu akili.

Ni vyema pia kusoma vitabu, vya elimu na maarifa na vitakatifu au kufanya mambo tofauti badala ya kukaa sehemu moja muda wote.

Shiriko hilo linahimiza kufanya mazoezi kila siku ili kupunguza kusononeka na kujiongezea furaha. Ni vyema pia kutafakari mafanikio yako na kujipatia nafasi ya kuishi bila kufikiria yajayo wala yaliyopita. Tena jisamehe nafsi yako.

Unaweza kukabiliana na msongo kwa kujipa muda wa kutosha wa kupumzika na kulala usingizi wa kutosha, wanasema wataalamu.

Kushirikiana na wengine na kuwasaidia ili nawe usaidiwe ni moja ya mbinu wanazozitaja za kukabiliana na msongo.

Pia wataalamu wanashauri kujenga tabia ya kushukuru kwa kila jambo, ulichonacho na kuweka orodha ya mambo unayoshukuru.

Wanashauri kufanyakazi unazozipenda ili ziwe kama mchezo na kila siku uzifurahie.

### KUMBUKA MAZOEZI

TANCDA wanashauri kuishi maisha ya mazoezi na kutaja baadhi ambayo unaweza kuyafanya nyumbani.

Mfano, wanasema ukiwa nyumbani kimbia mahali pamoja mfano kuzunguka sebuleni mara kadhaa, mengine ni kushuka na kupanda kwenye kiti. Aidha, unaweza kunyoosha na kuinua mgongo na kiuno. Piga goti kwa kubadilisha miguu, anza na kulia, maliza piga wa kushoto mara kadhaa.

Mengine ni kunyoosha mikono na kuizungusha mabegani kwenda mbele na kurudisha nyuma mara kadhaa pia.

Mazoezi mengine wanayopendekeza na wataalamu wa TANCDA ni kuchuchumaa na kunyanyuka, pia kupiga pushapu, jingine ni kulala chali kisha kutumia vidole vya miguu na mikono kujinyanyua juu.

Zoezi jingine ni kuruka juu mara kadhaa, kucheza kamba na vyote vifanyike kila mara.

Wanashauri kuwa kwa kuzingatia mazoezi na ushauri wa kitaalamu watu wengi watapunguza msongo na pia magonjwa yasiyoambukizwa kadhalika kubakia na afya njema.

ELIMU

NA WAANDISHI WETU

SIKU 16 UKATILI...

# Wazazi wakagueni watoto wenu acheni kuwaachia babu, bibi ulezi


Watoto wakihamasisha jamii kuwalinda dhidi ya ukatili. **PICHA: MWANDISHI WETU**

DUNIA inaendelea na Siku 16 za Harakati za Kupinga Ukatili wa Kijinsia kwa namna mbalimbali, watetezi wa haki za wanawake, wasichana na watoto wanasema ukatili na unyanyasaji umezidi.

Akizindua kampeni hizo nchini Sudan wiki iliyopita, Tom Fletcher, Mkuu wa Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kuratibu Misaada ya Dharura (OCHA), ana ujumbe kwa wanaume wanaowakatili kingono wanawake na watoto akisema:

"Nawaambia iwapo unadhani unafanya hivyo kwa sababu una nguvu, unakosea. Unafanya hivyo kwa sababu wewe ni dhaifu." Wanaume wanaofanya hayo ndiyo ujumbe wenu huo.

Kazi ya kupamba na ukatili, hapa nchini inaeleza kuwa upo mijini na vijijini ndani ya familia na ndugu wa karibu ndiko kwenye unyanyasaji zaidi.

Jamii inaamini kuwa nyumbani ni mahali salama kwa wanawake, wasichana na watoto lakini sivyo. Kuna shida. Ni kutokana na kuongezeka kwa ukatili kama unajisi wa watoto unaofanywa na wazazi, walezi na ndugu wa karibu kama baba mdogo na wajomba.

Udhalilishaji watoto wa kike na kiume, kukatili wanawake na wasichana kuwaua, baadhi wakikatishwa maisha na wapenzi au wenza ni matukio ya kila wakati.

Mkoani Pwani, Asasi ya 'Initiative for Domestic Workers', inafanya uhamasishaji wa ulinzi wa mtoto dhidi ya ukatili katika kata za Yombo na Fukayosi wilayani Bagamoyo.

Wakiwatembelea wanavijiji wa Matimbwa na Fukayosi kuhimiza ulinzi wa mtoto, anasema Ofisa Miradi Farida Jackson, akiongeza kuwa vitendo vya ukatili na jinai vinazidi.

Anaiambia Nipashe kuwa zama hizi watoto wa kiume wapo katika hatari ya kulawitiwa, wasichana nao wakinajisiwa na kuingiliwa kinyume cha maumbile nyumbani na kwenye jamii.

Anasema wamefanya mikutano ya mafunzo na wazazi na walezi wa Kata za Fukayosi na Yombo, wakiwahimiza kuwakagua watoto miili yao, kuangalia mabadiliko ya tabia na akili ili kugundua kama wanafanyiwa ukatili wa kijinsia mapema na kuwatafutia tiba.

"Pamoja na hayo tunawakumbusha anapokuja mgeni awe mjomba, baba mdogo au kaka asilale na watoto wao. Anaweza kuwadhalilisha," anasema Farida.

> Zama hizi kuna kampuni zinatafutia mabinti kazi za ndani na kuwapeleka kwa wanaowahitaji. Wazazi wanafuatilia? Wanawafahamu waajiri au aliyewasafirisha kutoka kijijini?

Anaongeza kuwa wapo ndugu wa karibu na wazazi ambao wametuhumiwa kunajisi watoto wa jamaa zao kwa kuwalawiti na kuwabaka na taasisi yao imepokea malalamiko ya mgeni anayeishi mjini anayefika Bagamoyo na kurubuni watoto kuwafanyia unyanyasaji.

Farida Ofisa Miradi anasema kazi hizo zinafanyika kwenye mradi wa kuwajengea uwezo wanawake, wasichana, watoto na jamii kuhusu kazi za staha kwa wafanyakazi za ndani ulioanza mwaka huu ukitarajiwa kukamilika Januari mwakani, ukidhaminiwa na Tanzania na Shirika linalofadhili miradi ya maendeleo ya wanawake (WFT-T).

Anasema kwenye mikutano wanawasisitiza wanavijiji waepuke mazoea ya kuruhusu watoto kwenda likizo kwa jamaa zao mikoani kwani mzazi au mlezi hajui mtoto wake anakutana na nani au nini na huenda anafanyiwa unyanyasaji kingono, kufunzwa uhalifu kama kutumia dawa za kulevya au pombe.

"Tumezungumzia madhara ya kuruhusu watoto kuishi na baba au bibi tukiwaambia leeni watoto wenu wenyewe, maisha ya sasa si kama ya zamani. Watu wanaweza kutumia mwanya wa uzee au hali ya kushindwa kufuatilia maendeleo ya watoto na kuwadhuru."

Anasema uhamasishaji unawataka wazazi au walezi waonyeshe msimamo katika malezi kwa kuwa wakali na kusimamia majukumu ya elimu, malezi na gharama wasiwaachie watu wengine.

**KAZI ZA NDANI MIJINI**

Akizungumzia mradi wa kuwajengea uwezo wanawake, wasichana, watoto na jamii kuhusu kazi za staha kwa wafanyakazi za ndani, Farida anasema wakazi wa vijiji vya Fukayosi na Yombo, ni miongoni mwa maeneo ambayo watoto wanakwenda kufanya kazi mijini baada ya kumaliza shule.

Anasema hilo nalo linazungumziwa na kuwambusha wazazi na walezi kuwa wengi hawatambui watoto wao wanafanya kazi kwa nani na katika mazingira gani.

"Zama hizi kuna kampuni zinatafutia mabinti kazi za ndani na kuwawapeleka kwa wanaowahitaji. Wazazi wanafuatilia? Wanawafahamu waajiri au aliyewasafirisha kutoka kijijini? "

Wanawahimiza wazazi kuwafahamu wanaowaajiri watoto wao tena kuthibitisha majina na vitambulisho vyao kwa kuingia mikataba na waajiri hao kwa ushahidi mahususi kwa viongozi wa serikali za vijiji na mitaa mahali walipo na vijijini walipotoka.

Anasema tumehimiza: "Tusione usumbufu, ni lazima kuwalinda watoto wetu, hata kama mzazi au mlezi hawezi kwenda, wanandugu wasaidiane, walimu wana maarifa mbalimbali wanaweza kutumika kutoa msaada na dawati la jinsia la kata na polisi kata na maofisa maendeleo ya jamii."

**KUJALI**

Farida anasema wazazi vijijini wanawageuza watoto wao kuwa vitega uchumi bila kujali madhira wanayopitia kwenye kazi wanazofanya mijini, mathalani, hawaulizi kuhusu mshahara, kazi wanazozifanya, na wengine hawana mawasiliano.

"Tuanze sasa kujua haya mambo kwa sababu nyakati zimebadilika, tusing'ang'anie kutumiwa mishahara kila mwezi, wala kutaka simu, mavazi na zawadi ambazo zinawaumiza mabinti wetu," anasema Ofisa Miradi Farida.

Anasema wanawahimiza wajali malalamiko ya watoto wao, mfano kufanyakazi bila mikataba, kunyanyaswa kingono, kutumikishwa kinyume na sheria, ujira mdogo au kukosa mshahara, vipigo na matusi.

Glady Kimathi, mwanaharakati wa kujitolea anayefanyakazi na Initiative for Domestic Workers, akizungumzia harakati hizo, anasema tafiti zimebaini kuwa baadhi ya wazazi wanawahamasisha watoto kufeli mitihani ya darasa la saba ili waende kufanya kazi za ndani mijini.

Anasema wametembelea shule za Fukayosi na Matimbwa kuwahimiza kufanya vizuri kwenye masomo yao ili kutimiza ndoto zao, wasome zaidi.

Anasema wanafunzi wamehimizwa kuripoti matendo ya unyanyasaji yanayofanywa nyumbani kwa walimu na wanapofanyiwa ukatili shuleni waripoti nyumbani.

Aidha, atika kata hizo, wanavijiji wametakiwa kuacha kufichiana siri za kihalifu hasa za udhalilishaji watoto, wanawake.

Anatoa mfano kuwa yapo mazoea kuwa mwanafamilia akinajisi mtoto, akishtakiwa itavunja undugu hivyo kuleta migogoro kwenye familia na kutengana.

Anaongeza kuwa shuleni pia wamewahamasisha wanafunzi kukataa kuingizwa kwenye mazingira hatarishi ambayo yatasababisha kunajisiwa au kubakwa, na wakifanyiwa vitendo hivyo maeneo ya shule waripoti nyumbani na ikiwa nyumbani waripoti shuleni.



## Waziri ahimiza ushiriki maonesho

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Ujenzi, Godfrey Kasekenya, amesema kuna umuhimu wa wananchi kujitokeza kwenye maonesho yanayoandaliwa, ili kupata elimu na kuchangamkia fursa zilizoko nchini za kujikwamua kiuchumi.

Alitoa rai hiyo juzi wakati akifunga maonesho ya makandarasi yaliyoandaliwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma.

Kasekenya alisema kwenye maonesho hayo wadau wamekuwa wakitoa elimu ya masuala mbalimbali kwa jamii na fursa hizo.

"Maonesho haya yamekuwa yakitoa fursa ya kuwafikishia wananchi bidhaa zinazozalishwa na kampuni mbalimbali pamoja na wajasiriamali," alisema.

Alieleza kuwa maonesho hayo yamekuwa yakiwakutanisha wajasiriamali na watu wenye viwanda kwa lengo la kutafuta soko kwa sababu wote wanategemeana.

Kadhalika, alisema katika maonesho hayo wajasiriamali wa uzalishaji wa mvinyo na wengine walipata fursa ya kukutanishwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Wakala wa Vipimo (WMA) ili kupata elimu ya kuzalisha bidhaa bora.

Alisema elimu itakayotolewa na mashirika hayo itawasaidia kununua bidhaa zenye ubora.

Mratibu wa maonesho hayo, Benard Mwata alisema wameshirikisha wajasiriamali wa ndani na nje ya nchi, ili kuongeza uwekezaji wa ujenzi katika maeneo mbalimbali nchini.

Alisema watoa huduma hao za ujenzi wamesaidia kuwainua wajasiriamali ili wakue na kuanzisha kampuni zitakazotoa ajira kwa watu wengine.

Ofisa Biashara Mkoa wa Dodoma, Amri Kibwana, alisema Ofisi ya Mkuu wa Mkoa huo wataendelea kuandaa maonesho mengine kwa lengo la kuwajengea uwezo wazalishaji wa bidhaa za mvinyo wajasiriamali mkoani hapa.

# Askofu awapa ujumbe viongozi serikali za mitaa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Karmeli Assemblies of God Tanzania, Dk. Evance Chande, amewataka wenyeviti wa serikali za mitaa waliochaguliwa kujiepusha na rushwa na kutatua kero za wananchi kwa vitendo bila ubaguzi.

Dk. Chande aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kumalizika kwa ibada iliyofanyika katika kanisa hilo lenye makao makuu yake Ipagala mkoani Dodoma.

Alisema wananchi waliowachagua wana imani na wao, hivyo kwa kupitia ilani za vyama vyao wanawategemea kutatua kero walizokuwa nazo kwa vitendo kwa kushirikiana na serikali.

Aidha, alisema viongozi hao ni tegemeo la wananchi, hivyo wanapaswa kutoa huduma na bila kupokea rushwa.

"Ni matarajio ya wananchi walio wengi tukiwamo sisi viongozi wa dini ni imani yetu wale wote waliochaguliwa kushika nafasi hiyo ya uenyekiti wa Serikali za Mitaa na Vijiji, Vitongoji watajitoa kwa moyo wote na watawatumikia katika kuhakikisha wananchi wanaondokana na kero," alisema.

Hata hivyo, alisema ili kufanikiwa katika utendaji wao wenyeviti hao wanatakiwa pia kuondoa utofauti waliokuwa nao wa kwenye vyama vya siasa, badala yake waungane na wananchi kwa kufanya kazi ili kuleta maendeleo ndani ya maeneo yao.

Kadhalika, aliwaasa viongozi hao kumsaidia Rais Samia Suluhu Hassan katika kutatua kero mbalimbali na kuwasaidia wananchi kuzisemea kwa serikali.

Pia, aliwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa viongozi waliochaguliwa ili kuleta mafanikio ya kimaendeleo ya kiuchumi kwenye maeneo yao.



Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani Tanzania, Saidi Ally Mohamedi, akipanda mti katika Shule ya Msingi Mleni, jijini Tanga mwishoni mwa wiki, ikiwa ni mwendelezo wa kitaifa wa maadhimisho ya miaka 50 ya baraza hilo. Kulia ni Ofisa Elimu ya Awali na Msingi wa Jiji hilo, Shomari Bane. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Mil.40/ kuwajengea uwezo wanawake wenye ulemavu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ZAIDI ya Sh. milioni 40 zimetolewa na shirika lisilo la kiserikali la Abilis Foundation kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kuwajengea uwezo wanawake vijana wenye ulemavu kwenye masuala ya uongozi wilayani Kondoa mkoani Dodoma, ili kukuza demokrasia nchini.

Mradi huo unatarajiwa kutekelezwa na shirika la kuhudumia watu wenye ulemavu Dodoma la FDH na zaidi ya watu wenye ulemavu 300 watarajiwa kufikiwa.

Mkurugenzi wa FDH, Michael Salali alisema hayo jana jijini hapa wakati akitambulisha mradi huo kwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma kwa ajili ya utekelezaji.

Alisema lengo la mradi huo ni kuwajengea uwezo wanawake vijana wenye ulemavu kuchangamkia fursa za uongozi katika jamii yao na kuondokana na tabia ya kujinyanyapaa wenyewe.

"Mafunzo tutakayotoa yatasaidia kundi hili kuondokana na dhana potofu ya wenye ulemavu kujichukulia kuwa wao hawezi kuwa viongozi, badala yake wajitokeze kwa wingi kukamata fursa zote za uongozi zinazojitokeza mbele yao," alisema.

Aliongeza kuwa: "Mradi huu wa mwaka mmoja sisi FDH tunakwenda kutekeleza lakini fedha za ufadhili ni kutoka Abilis Foundation shirika lenye makao makuu yake nchini Finland lakini hapa nchini ofisi zao zipo jijini Arusha."

Aidha, alisema mradi huo unakwenda kugusa makundi yote ya watu wenye ulemavu kwa ajili ya kuwajengea uwezo kwenye masuala ya uongozi na kukuza demokrasia pamoja na ujasiriamali.

"Leo tumekuwa na kikao na viongozi kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma ambao ni wajumbe wa CHMT, lengo likiwa kwanza kuutambulisha mradi lakini pia uelewa kwa sababu serikali na sisi kama wadau tunafanya kazi kwa pamoja, hivyo hatuwezi kwenda kutekeleza mradi kama huu bila serikali kuufahamu na kutoa ushirikiano wake," alisema.

Aidha, aliahidi kwenda kutekeleza kile ambacho kimekusudiwa kwenye mradi huo na siyo vinginevyo, ili kupata matokeo chanya na jamii ya watu wenye ulemavu.

Alisema: "Kwanza mradi huu tunatarajia kuwafikia moja kwa moja watu 300 kwenye Kata ya Kilimani, Chemchem na Bolisa lakini pia makundi mengine katika jamii kupitia uhamasishaji wa vipindi vya redio na mikutano mbalimbali tutakayoifanya kwenye Halmashauri ya Kondoa".





# Madaktari bingwa watua Njombe, RC awaita wananchi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, ametoa rai kwa wananchi mkoani humo kujitokeza kwa wingi ili kupata matibabu ya magonjwa kutoka kwa madaktari bingwa na bobezi 32 katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Njombe.

Alitoa rai hiyo jana wakati wa uzinduzi wa kambi ya madaktari bingwa wa Rais Samia iliyofanyika katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Njombe RRH.

Mtaka alisema ni vema jamii mkoani humo ikaweka utaratibu wa kupima afya zao ili kuondokana na vifo vya ghafla ambavyo vinaweza kuepukika.

"Sasa ninawaambia wananchi mkoani Njombe madaktari bingwa wa Samia wapo kwenye hospitali yetu, nitumie nafasi hii kuwaalika wananchi wote ambao wanachangamoto za afya watumie fursa hii ya siku tano kuja kupata matibabu," alisema Mtaka.

Mtaka alisema kuwa jambo zuri ni kwamba matibabu hayo yanafanyika mwishoni wa mwaka ambapo mara nyingi wanashauri kufanya uchunguzi wa afya zao.

"Unapofunga mwaka pamoja na maangaiko yako yote lakini umepata nafasi ya kujiangalia, huduma hii imekuja Njombe niwaombe wananchi wachangamkie hii huduma kwa sababu mtaji mkubwa wa binadamu ni afya," alisema Mtaka.

Awali Mkurugenzi wa Tiba kutoka Wizara ya Afya, Dk. Hamad Nyembea, alisema lengo la wizara katika kambi hizo ni kutekeleza mikakati ya serikali hasa namba tano wa sekta ya afya ambao umeelekeza upatikanaji wa huduma za afya za msingi lakini pia za kibingwa kwa wananchi wote.

"Tunafahamu kambi hizi zipo aina mbili na aina ya kwanza ni ile ambayo imeshafanyika tayari ambayo ilizihusisha halmashauri zote nchini ambapo halmashauri 184 ziliweza kufikiwa na mabingwa," alisema Dk. Nyembea.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Njombe, Dk. Gilbert Kwesi, alisema ujio wa madaktari unaleta ahueni kwa wananchi kwa sababu ya kuepuka gharama ambazo wangetumia kufuata huduma hizo nje ya mkoa hususani Hospitali ya Taifa Muhimbili iliyoko jijini Dar Es Salaam.

"Kipindi hiki cha kambi kwa siku tano tunategemea gharama zitakuwa ni za uchangiaji lakini wale wenye bima za afya zinapokelewa na gharama siyo kubwa, hivyo wananchi waje ili wapate huduma," alisema Kwesi.

Mmoja wa wananchi mjini Njombe, akiwamo Selina Mwinuka aliishukuru serikali kwa kuleta madaktari hao ambao watasaidia kuwaondolea adha ya kwenda kufuata huduma hizo nje ya Mkoa wa Njombe.



Meneja Miradi Hospitali ya CCBRT, Yohana Kasawala (wa pili kushoto), akifafanua jambo kwa mabalozi wa fistula wapatao 50 kutoka mikoa mbalimbali nchini, wakati wa mkutano wao wa mwaka uliofanyika hospitalini hapo, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: JOHN BADI**

## CCM Njombe yapata ushindi wa asilimia 99.7 uchaguzi S/mitaa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Njombe kimefanikiwa kushinda Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa asilimia 99.7.

Katika uchaguzi huo uliofanyika Novemba 27, mwaka huu, CCM Mkoa wa Njombe ilipata vijiji 377 kati ya 381, mitaa 81 kati ya mitaa 82 na vitongoji 1819 kati ya 1,832.

Hayo yalielezwa juzi na Katibu wa Siasa Uenezi na Mafunzo wa CCM Mkoa wa Njombe, Josaya Luoga, wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Alisema kazi nzuri waliyoanza kuifanya tangu uchaguzi uliopita wa mwaka 2019 imewajengea imani kubwa na kusababisha wananchi kuwachagua tena kwa kishindo ikiwa ni ishara ya kwenda kufanya vyema katika uchaguzi mkuu ujao.

Luoga alisema katika nafasi za wajumbe mchanganyiko wa serikali za vijiji 3,710, CCM imepata wajumbe 3,698 jambo linaloonesha kuwa chama hicho kinakubalika zaidi na kuaminika katika jamii.

Kutokana na ushindi huo CCM kimepongeza jitihada za wananchi kukiamini chama hicho na kuwataka kwenda kushirikiana vyema na viongozi waliowachagua katika kujiletea maendeleo.

Aidha, aliwataka waliochaguliwa kwenda kusimamia shughuli za maendeleo na miradi inayoendelea kwenye maeneo yao kwa kufuata utaratibu, sheria na kanuni zilipo, ili kufanikisha maendeleo kwenye jamii zao kuliko kutumia nafasi walizopata kujinufaisha na kuwanyanyasa wananchi.

Alisema chama hicho hakitoi maelekezo kwa wenyeviti kwenda kutoza fedha kwa ajili ya muhuri kwa wananchi, badala yake wakatoe huduma huku akitoa tahadhari kuwa wasidhani wanakwenda kupata fedha kwa kuwa kazi hiyo ni ya kujitolea.

# DC: UKIMWI bado upo, chukueni tahadhari

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WANANCHI mkoani Mbeya wametakiwa kuendelea kujikinga na kuchukua tahadhari ya ugonjwa wa UKIMWI kwani bado upo licha ya juhudi zinazoendelea kufanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mbarak Batenga, alitoa wito huo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya wakati wa maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani yaliyofanyika juzi wilayani humo.

Batenga alisema msingi wa kwanza wa mtu ni kuwa na afya njema kwani maendeleo pesa na mambo mengine yanapatikana kwa kuwa na afya njema na kwamba licha ya kuwapo dawa za kufubaza makali ya VVU lakini bado tiba na chanjo ya ugonjwa huo bado haijapatikana.

"Tiba ya UKIMWI bado haijapatikana wala chanjo, tukilitambua hilo tutaendelea kujikumbusha kwamba UKIMWI bado upo, hivyo tuishi kwa kujikinga na kuchukua tahadhari, tuepuke tabia hatarishi zinazoweza kusababisha kupata maambukizi," alisema Batenga.

Aliwataka wananchi kuendelea kujitokeza kupima afya zao ili watakaogundulika kuwa na maambukizi waanze kutumia dawa za kufubaza makali ya VVU pamoja na kupata mbinu za kuepuka maambukizi mapya.

Pia, alitoa wito kwa wanaume kujitokeza kupima afya zao badala ya kutegemea vipimo vya wake zao, kwamba majibu ya wake zao ndiyo majibu yao kwani jambo hilo siyo sahihi na kwamba afya ni jambo la mtu binafsi na siyo jambo la familia.

"Wanaume acheni kutembea na majibu ya vipimo vya wake zenu hasa yanapokuja majibu mazuri, hiyo kwani anayepata ugonjwa huu ni mtu na siyo familia, mke anaweza kuwa mzima na wewe ukawa na maambukizi, hivyo kila mtu akapime yeye mwenyewe ajue afya yake," alisisitiza.

Awali akitoa salamu katika maadhimisho hayo, Diwani wa Kata ya Ifumbo, Weston Mpyila alishukuru maadhimisho hayo kufanyika katika Wilaya ya Chunya kimkoa, akisema imekuwa nafasi nzuri ya wao kujifunza kupitia mada mbalimbali kutoka kwa wadau na wataalamu.

Akisoma taarifa ya hali ya utoaji wa huduma za VVU na UKIMWI Mratibu wa Huduma za UKIMWI Mkoa wa Mbeya, Dk. Deo Magongwe, alisema lengo la maadhimisho hayo ni kuongeza uelewa katika jamii na kuijulisha jamii kufahamu mafanikio na vikwazo vinavyoikabili dunia.





# Z'bar ina hekta 37,800 za misitu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo kupitia Idara ya Misitu imesema Zanzibar ina eneo la misitu lenye ukubwa wa hekta 37,801.38, kati ya hiyo Unguja ni 22,137.38, Pemba ni 15,664.

Imesema hatua hiyo ni baada ya kufanya utafiti uliolenga kubaini kiwango cha misitu iliyopo Zanzibar mwaka 2013.

Waziri wa Wizara hiyo, Shamata Shaame Khamis, alisema hayo juzi katika Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na mwakilishi wa Mtambwe, Dk. Muhammed Ali Suleiman.

Mwakilishi huyo alitaka kujua tathmini ya sensa ya miti iliyopo hivi sasa kwa uoto wa asili, misitu na mikarafuu, pamoja na ni changamoto zipi ambazo serikali imekumbana nazo hadi kushindwa kufanya sensa hiyo ya miti.

Akijibu swali hilo, Shamata alisema katika kipindi cha miaka 16 kuanzia mwaka 1997 hadi 2013, misitu ya mikoko imepungua ujazo kutoka mita 41.0 hadi 18.9 kwa upande wa Unguja na kwa Pemba imepungua kutoka mita 39.8 hadi mita 38.3.

Waziri Shamata alisema sensa ya miti hufanyika kwa matakwa ya kisheria ambapo Sheria ya Rasilimali za Misitu ya Mwaka 1996 Kifungu Namba 5(b) inamtaka Msimamizi Mkuu wa Misitu kufanya sensa ya miti kwa lengo la kutambua aina na kiwango cha rasilimali za misitu kilichoko.

Alisema kwa kawaida sensa ya miti hutakiwa kufanyika kila baada ya miaka 10 ambapo kipindi hicho mabadiliko, ongezeko na upunguaji wake huweza kutambuliwa ili hatua ziweze kuchukuliwa.

"Sensa ya miti kwa hapa Zanzibar imeweza kufanyika kwa awamu mbili zikiwamo ya mwaka 1997 na 2013, sensa ya miti ni nyenzo muhimu katika ustawishaji wa hali ya kimazingira ya nchi ambayo inahitaji mtaji mkubwa wa rasilimali fedha, watu pamoja na teknolojia," alisema.

Aidha, alisema kwa uzoefu wa sensa iliofanywa mwaka 2013 iligharimu Sh. bilioni 1.2 na mara nyingi fedha hizo hutegemea kutoka kwa wahisani.

Alisema juhudi kubwa zinafanyika ili kuweza kupata fedha kwa ajili ya sensa ya miti na hivi karibuni Wizara ya Kilimo Zanzibar kwa ushirikiano na Wizara ya Maliasili na Utalii ya Serikali ya Tanzania ilikutana kwa ajili ya lengo la kutayarisha andiko la mradi wa pamoja kwa ajili ya kuomba fedha.

Katika hatua nyingine, Shamata alisema ni kweli Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliahidi kuongeza idadi ya mifumo ya umwagiliaji maji ili kuwasaidia wakulima kuondokana na kilimo cha mazoea.

Alisema ukubwa wa eneo la umwagiliaji limengezeka kutoka hekta 875 mwaka 2019 hadi kufikia hekta 2,300 mwaka 2024.

Alisema kuhusu idadi ya wakulima wanaonufaika na kilimo cha umwagiliaji hadi sasa maeneo ya kilimo cha umwagiliaji maji yana ukubwa wa hekta 2,300 ambazo ni takribani asilimia 23 tu ya eneo lote.

Aidha. alisema kwa kuzingatia umuhimu wa kilimo cha umwagiliaji, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo inaendelea na jitihada zake za kuyaendeleza maeneo mapya ya umwagiliaji na kukarabati miundombinu iliyochakaa.



Mwakilishi wa Jimbo la Mwanakwerekwe, Ameir Abdallah Ameir, akizungumza wakati wa kipindi cha maswali na majibu katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani, Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Serikali kuongeza vivutio vya utalii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Utalii na Mambo ya Kale imesema kuwa inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuongeza vivutio vya utalii nchini.

Waziri wa Wizara hiyo, Mudrik Ramadhan Sora, alivitaja baadhi ya vivutio hivyo ni Rasi Mkumbuu kwa Pemba, Kwa Bi Khole - Bungi, Pango la Mangapwani, Kasri ya Mwinyi Mkuu Dunga kwa Unguja.

Aliyasema hayo jana wakati akijibu swali aliloulizwa na mwakilishi wa Mwanakwerekwe, Ameir Abdallah Ameir katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Ameir alitaja kujua kwa kiasi gani wizara hiyo inatoa msukumo katika taasisi mbalimbali ikiwa ni pamoja na taasisi maarufu ya 'Karibu Zanzibar Festival' katika kukuza utalii nchini.

Akijibu swali hilo, Waziri Soraga alisema vivutio hivyo ni sehemu ndogo ya vivutio vilivyopo Zanzibar na wizara yake inaendelea na juhudi za kuvitangaza na kuvirejesha na kuvihuwisha kurudi katika hali yake ya asili.

Aidha alisema wizara yake kupitia Kamisheni ya Utalii huzisaidia taasisi mbalimbali katika kuwapa fedha, miongozo na kujitangaza.

Aidha, Soraga alisema Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale iko tayari kufanya ushirikiano na taasisi zote zenye malengo mapana ya kuchochea maendeleo ya utalii wa Zanzibar.

Hata hivyo alisema Wizara ya Utalii kupitia Mamlaka ya Mji Mkongwe imeingia mkataba wa ubia pamoja na jumuiya ya hifadhi kwa ajili ya ukarabati wa jengo hilo.

# Biteko: Tuzo za waajiri zinaleta uhusiano mzuri kazini

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Mkuu, Dk. Doto Biteko amesema tuzo za Shirikisho la Waajiri Tanzania (ATE) ni kichocheo muhimu cha ushindani kati ya waajiri kuboresha masharti ya kazi, ikiwemo usalama kazini.

Amesema pia ni kichocheo cha kuongeza viwango vya juu vya uzalishaji na uhusiano mzuri kati ya waajiri na wafanyakazi kwa maendeleo ya kampuni au mashirika yao.

Dk. Biteko alisema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa mgeni rasmi katika tuzo za mwajiri bora wa mwaka zilizoandaliwa na ATE.

Dk. Biteko ambaye ni Waziri wa Nishati, aliwahimiza washiriki kudumisha viwango vya juu vilivyowawezesha kufikia mafanikio pamoja na kuendelea kuweka viwango vya ubora katika maeneo yao ya kazi.

"Nawapongeza ATE kwa mpango huu unaolenga kuboresha masharti ya kazi kwa waajiri katika maeneo ya kazi na tunaamini mtaendelea kuchochea ushindani kati ya waajiri ili waendelee kujitahidi," alisema Dk. Biteko.

Tuzo hizo ni mpango wa ATE na zimekuwa zikifanyika kila mwaka tangu zilipoanzishwa mwaka 2005, lengo likiwa ni kuinua rasilimali watu ili ziweze kutekeleza jukumu lao kuu katika utendaji wa biashara.

Tuzo hizo zinategemea utafiti wa kisayansi na wa kitaalamu kuhusu usimamizi wa rasilimali watu na uongozi katika mashirika makubwa na biashara ndogo na za kati zinazokua haraka, kwamba kwa mwaka huu kampuni zaidi ya 100 na mashirika yalishiriki.

Mkurugenzi Mtendaji wa ATE, Suzanne Ndomba-Doran alisema kuwa tuzo hizo zilianzishwa ili kutambua waajiri ambao ni wanachama wa ATE na wanaofanikiwa katika kutekeleza mikakati madhubuti inayokuza usimamizi wa rasilimali watu na shughuli za biashara.

"Tangu kuanzishwa kwake, tuzo hizi zimeendelea kuchochea makampuni kuwekeza katika maeneo haya kwa kufuata sheria, kuanzisha sera, kanuni na mazingira rafiki ya kuboresha tija na ushindani," alisema.

Akizungumza baada ya kupokea tuzo kwa niaba ya AOTTL, Mkurugenzi wa Rasilimali Watu wa AOTTL, Blasius Lupenza, alieleza fahari yake kwa uongozi kwa kuboresha sera na utamaduni wa kazi wa kampuni.

Alisema wanajivunia kushinda kipengele cha ajira na uongozi, kwamba tuzo hiyo ushuhuda wa michango yao ya kipekee.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**GOODTIME SAMBURA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye Index No. 0534/0139 Kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia ST.ANTHONY'S SECONDARY SCHOOL mwaka 2009. Cheti cha kidato cha Sita chenye Index No. S/0534/0708 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia ST. ANTONY'S SECONDARY SCHOOL mwaka 2012.Cheti UNIVERSITY OF DODOMA Chenye Namba T.UDOM.2021.00400 mwaka 2015. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi **:PHQ/DAR/KIN/229888/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**IBRAHIMU YUSSUPH MTEMILE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye Index No. S2574/0046 Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MIBUYUNI SECONDARY SCHOOL mwaka 2020. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi **:PHQ/DAR/TEM/92861/2024**

## KUPOTEA KWA VYETI



**TEKLA PASCAL MZIBA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye Index No. S2391/0065 Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia LUDUGA SECONDARY SCHOOL mwaka 2017.Cheti cha CHUO CHA MAENDELEO YA JAMII RUNGEMBA (NTA 4) Chenye Namba S2391/0065/2017 mwaka 2020.Cheti cha CHUO CHA MAENDELEO YA JAMII RUNGEMBA (NTA 5) Chenye Namba S2391/0065/2017 mwaka 2021. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi **:PHQ/MOR/KIL/41305/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JUNIOUR PHABIAN MBUYA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye Index No. S2379/0323 Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MAJANI YA CHAI SECONDARY SCHOOL mwaka 2020. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi :**PHQ/DAR/ILA/263679/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**WEMA NG'ELENGE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye Index No. S1603/0084 Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia NYOLOLO SECONDARY SCHOOL mwaka 2007. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi **:**
**PHQ/NJO/MAK/2401/2024**

## KUPOTEA KWA VYETI



**ASHA JOSEPH** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye Index No. S0713/0010 Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia IGUNGA SECONDARY SCHOOL mwaka 2012. Cheti cha kidato cha sita chenye Index No. S0348/0505 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia TUMAINI SECONDARY SCHOOL mwaka 2015. Cheti cha Chuo Kikuu Kishiriki cha Dar es Salaam (DUCE) chenye Namba D.BAED0004792 mwaka 2018. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi **:PHQ/DAR/UBU/265049/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**HASSAN NASSOR MBIKI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.2426/0028 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **CHAMAZI ISLAMIC** mwaka 2010. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/MWA/NYA/45793/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ASAJILE CLINTON** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye Index No. S1377/0218 Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia NATIONAL CORRESPONDENCE INSTITUTE CENTRE mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi :PHQ/DAR/ILA/264925/2024

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 29639 OF 2024**
**In the matter of the Estate of the late CHARLES DENNIS MKUDE of Ilazo Street in Ipagala ward within Dodoma City Council.**
**In the matter of an application for Letters of administration by EVA TENGIO URIO**
**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 18 Day of 12...2024
Dated at Dodoma this 2 Day of 12 2024.

..........................................................................
**PETITIONER**
**Presented for filing thi day of 2024**

**REGISTRY OFFICER**

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**RIET ELIBARIKI MOSHI**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 530 ANR Chasses Namba IN46-0001864, Engine Namba IQ433624. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Polisi Taarifa:
**DAR/KIJ/RB/467576/2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**
**IDARA YA UHAMIAJI**
**Hii ni kwa taarifa kwamba:**
**MR. GEORGE EL TAYYAR**
**P.O. Box 184, MASASI - MTWARA**



Mwenye picha hapo juu, anaomba uraia wa Tanzania kwa Mh. Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi, utaifa wake kwa sasa ni MLEBANONI. Nchi atokayo ni LEBANON. Shughuli zake ni MFANYABIASHARA na anwani yake ni S.L.P 184 MASASI, MTWARA. Yupo hapa hapa nchini tangu mwaka 2014. Kwa yeyote mwenye taarifa/sababu za kwanini mwombaji asipewe uraia wa Tanzania, atume taarifa ya maandishi kwa Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, S.L.P 512 Dar es salaam.

**KUMB. NA. DN.........................**
**KNY: KAMISHNA JENERALI WA UHAMIAJI**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ERASTO ISRAEL** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye Index namba P368/596 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia IMBORU Secondary school Centre mwaka 2009. Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.**TAARIFA YA POLISI: PHQ/MAN/BAB/11049/2024**

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(TANGA SUB-REGISTRY)**
**AT TANGA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.24266 OF 2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE REMENCY SHIKUSIRIAEL TARIMO**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR GRANT OF LETTERS OF ADMINISTRATION BY DANIEL REMENCY TARIMO**
**GENERAL CITATION**
**(Made Under Rule 75 of the Probate Rule)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named petitioner.
The petition has been fixed for Hearing on 03rd Day of December, 2024 before Hon. M.J CHABA, J.
Objections to the grant should be filed on or before the 03rd Day of December, 2024
Dated at Tanga this 14th Day of November, 2024.

Deputy Registrar
TANGA

## KADI ZA GARI IMEPOTEA

Ndugu **PERPETUA TITUS MSOKA** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari yenye usajili ufuatao; T.725 ATK Chasis Na. SALLNABA7WA621655. Kwa yeyote atakayeona anaombwa kutoa taarifa kwenye kituo chochote cha Polisi kilicho karibu. Taarifa Polisi:
**PHQ/DAR/KIN/264818/2024**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KITUO MIKINDANI MKOA WA MTWARA**
**SHAURI LA MADAI/NDOA NA 183/2024**
**JINA LA MDAI MRASA HERMAN MBOTE**
**NA**
**JINA LA MDAIWA MARTH EDSON MBUYA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za Utaratibu madai katika mahakama za mwanzo)**
**KWA MARTH EDSON MBUYA WA DAR ES SALAAM**
**KWA KUWA MADAI/WADAI AMELETA/WAMELETA MADAI YAKE/YAO KWAMBA (ELEZA HAPA AINA YA MADAI) MADAI YA PESA TSHS. 3,380,000/=**
**KWAHIYO:** Unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama tarehe 04 Mwezi 12 Mwaka 2024 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa hayona kwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO: Kama hutohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati yakuitwa mahakamani inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 29 Mwezi 11 Mwaka 2024

.............................................
HAKIMU
HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO WILAYA YA MTW KITUO MIKINDANI


**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710. E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***
***Tupigie: +255 - 0677 020701***

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

## Senegal kuihoji Ufaransa mauaji wanajeshi wake

**DAKAR,** Senegal

SENEGAL imeadhimisha kumbukumbu ya miaka 80 ya mauaji ya wanajeshi wa Kiafrika waliopigania Ufaransa wakati wa Vita vya Pili vya Dunia, ambao waliuawa kwa kupigwa risasi na wanajeshi wa Ufaransa mwaka 1944 kwa kudai kutendewa haki na malipo waliporejea.

Nchi hiyo ya Afrika Magharibi kwa muda mrefu ilikuwa ikimtaka mkoloni wake wa zamani kuwajibika, kuomba radhi rasmi na kuchunguza ipasavyo mauaji yaliyotokea huko Thiaroye, kijiji cha wavuvi nje kidogo ya mji mkuu wa Senegal, Dakar.

Maadhimisho hayo, ambayo yalifufua madai hayo, yalifanyika wakati Ufaransa ikipoteza ushawishi kwa makoloni yake ya zamani ya Afrika, ambayo mengi yamegeukia Russia kwa usalama badala yake.

Rais wa Senegal, Bassirou Diomaye Faye, aliwaambia wageni na waandishi wa habari. "Wapiganaji wa Kiafrika walijitolea kwa kila kitu. Walitoa ujana wao, damu yao na nyama yao kwa ajili ya uhuru na amani ya dunia."

Ilielezwa kuwa kumbukumbu za mauaji hayo zinatofautiana, sawa na idadi ya waliouawa, ambayo rais wa zamani wa Ufaransa Francois Hollande aliiongeza hadi takriban 70 kutoka 35 wakati wa ziara yake mjini Thiaroye mwaka 2014.

Aidha, wanahistoria wanasema huenda mamia walikufa katika makabiliano na mamlaka ya kikoloni.

Sherehe hiyo ambayo waziri wa mambo ya nje wa Ufaransa alihudhuria pamoja na wakuu wengine wa nchi za Afrika, ilianza kwa kutembelea makaburi ya kijeshi ya Thiaroye kuweka maua. Ilielezwa kuwa mwongozo uliochapishwa wa sherehe hiyo ulielezea ukandamizaji wa kutisha wa wanajeshi wa kitengo cha Waafrika wa Senegal, ambao walizingirwa na kupigwa risasi kwa kuomba fidia inayostahili.

Siku chache kabla ya maadhimisho hayo, Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron aliandika barua kwa umma kwa mwenzake wa Senegal Faye ambako alitaja kitendo cha wanajeshi hao kupigwa risasi kuwa yalikuwa ni mauaji. Faye alisema kukiri kwa Macron ni hatua muhimu katika mchakato wa kurejesha heshima na utu wa waathiriwa.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Ufaransa, Jean-Noel Barrot, alisema katika hotuba yake kwamba nchi yake imetambua kuwa siku hiyo, msururu wa matukio ulianzishwa na kusababisha mauaji.

Gaspard Mbaye, ni Mkuu wa chama kinachojishughulisha na kumbukumbu za wanajeshi hao, aliambia Reuters kuwa amesikitishwa kwa sababu alitarajia zaidi kutoka kwa serikali ya Ufaransa. **TRT**

# Biden amsamehe mwanawe Hunter mashtaka ya jinai



Rais Joe Biden (kushoto), akiwa na mwanawe Hunter (kulia). **PICHA: REUTERS**

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Joe Biden, amempa mwanawe Hunter Biden msamaha wa rais na kumwepushia kifungo jela kutokana na makosa ya umiliki wa bunduki kinyume cha sheria na madai ya kukwepa kulipa kodi.

Kwa hatua hiyo, Rais Biden amekwenda kinyume na ahadi yake ya awali ya kutotumia nguvu zake za urais kwa manufaa ya familia yake.

Katika taarifa iliyotolewa jioni ya jana Rais Biden alisema, "nauamini mfumo wa sheria, ila kwa kuwa nimepambana na hili, naamini pia kwamba siasa zimeingia kati katika kesi hii na zimepelekea kutopatikana kwa haki."

"Madai katika kesi yake yametokea tu baada ya wapinzani wangu kadhaa wa kisiasa katika Congress kuyatumia kunishambulia na kupinga kuchaguliwa kwangu," aliongeza Biden.

"Hakuna mtu yeyote mwenye busara atakayeutazama ukweli katika kesi ya Hunter, atakayefikia maamuzi mengine mbali na kuwa Hunter alilengwa kwa kuwa ni mwanangu. Natumai raia wa Marekani wataelewa kwanini baba na rais atafikia uamuzi huu," alisema Rais Biden.

Hayo yanajiri wakati ambako Hunter Biden alikuwa anatarajiwa kuhukumiwa katika wiki chache zijazo na chini ya miezi miwili kabla rais mteule wa Marekani Donald Trump kuchukua hatamu za uongozi.

Hatua hiyo inafikisha mwisho gumzo la muda mrefu kuhusiana na mwanawe Biden, ambaye mwezi mmoja baada ya babake kushinda uchaguzi wa mwaka 2020, alifichua hadharani kwamba alikuwa anachunguzwa.

Ilielezwa kuwa Rais Biden aliapa mbele ya Wamarekani mara kadhaa kwamba ataheshimu utawala wa sheria baada ya muhula wa kwanza wa Trump, ila kwa sasa inadaiwa kuwa amekwenda kinyume na ahadi hiyo.

Mwezi Juni, Biden aliondoa uwezekano wa kumsamehe mwanawe au kupindua uamuzi wa mahakama, akiwaambia waandishi wa habari wakati Hunter alipokuwa akikabiliwa na kesi hiyo ya umiliki wa bunduki huko Delaware kwamba, "naheshimu uamuzi wa majaji. Nitafanya hivyo na sitamsamehe."

Novemba 8, mwaka huu baada ya ushindi wa Trump, msemaji wa ikulu ya White House Karine Jean-Pierre aliondoa uwezekano wa msamaha kwa Hunter akisema, "tumeulizwa swali hili mara kadhaa. Jawabu letu bado ni lile lile, hapana."

Hata hivyo, ilielezwa kuwa Rais Biden amekuwa akimuunga mkono mwanawe wa pekee wa kiume aliye hai, kwani Hunter aliingilia matumizi ya dawa ya kulevya na kuyaharibu maisha yake na ya familia yake, kabla ya kujiondoa kutoka kwenye matumizi ya dawa hayo katika miaka ya hivi karibuni.

Ilielezwa kuwa kwa miaka sasa, wapinzani wa kisiasa wa Biden wamekuwa wakiyatumia makosa ya mwanawe kumshambulia na kumkosoa.

Vile vile, Hunter Biden alifunguliwa mashtaka mwezi Juni katika mahakama ya shirikisho ya Delaware kwa makosa matatu ya kununua bunduki mwaka 2018, huku waendesha mashtaka wakisema, alitoa taarifa ya uongo kwenye fomu aliyoijaza akidai kwamba alikuwa hatumii mihadarati kinyume cha sheria au alikuwa si mraibu wa dawa hayo ya kulevya.

Pia ililelezwa kuwa mwezi Septemba, alifikishwa kizimbani jimboni California akituhumiwa kutolipa kodi ya angalau dola milioni 1.4. Na kwamba alikiri mashtaka hayo katika hatua iliyowashangaza wengi, saa kadhaa kabla majaji wa kusikiliza kesi yake kuanza kuchaguliwa. **APE/AFP/DW**

# Bado kitendawili hatima udhibiti plastiki

**BUSAN,** Korea Kusini

MKUTANO wa Umoja wa Mataifa (UN) kuhusu taka za plastiki uliokuwa unafanyika kwenye mji wa Busan nchini Korea Kusini, umetamatika huku wajumbe wakishindwa kufikia makubaliano ya mkataba wa kidunia kuhusu udhibiti wa taka za plastiki, ambako wamekubaliana kuongeza muda wa majadiliano.

Ilielezwa kuwa kwa karibu wiki moja, wanadiplomasia kutoka mataifa takribani 200 walikuwa wakijaribu kutafuta muafaka wa pamoja kuhusu namna ya kukabiliana na athari za taka za plastiki.

Katika kongamano hilo, mataifa ya Afrika yalikuwa yanaunga mkono kupatikana kwa mkataba wa kidunia kudhibiti taka za plastiki, lakini zikakutana na upinzani toka mataifa ambayo ni wazalishaji wakubwa wa mafuta ya Visikuku, yanayopinga azimio lolote la kusitisha uzalishaji wa plastiki.

Miongoni mwa masuala tata yaliyokwamisha makubaliano hayo ni pamoja na ni vipi kutakuwa na udhibiti wa uzalishaji wa plastiki zisizo na tija, aina ya kemikali zinazotumiwa, ufadhili wa kifedha kwa nchi masikini pamoja na kuwa na sheria ya kimataifa itakayofuatwa na mataifa yote duniani kuhusu taka za plastiki.**RFI**

# KOCHA AZAM ATOA SIRI YA USHINDI MECHI 7 MFULULIZO

Na Adam Fungamwango

KOCHA Mkuu wa Azam FC, Rachid Taoussi, amesema siri ya ushindi wa michezo yake saba mfululizo ya Ligi Kuu ni kuwa na wachezaji wazoefu na wavumilivu uwanjani, huku pia akijua staili gani ya kucheza kwenye viwanja husika.

Akizungumza juzi baada ya timu yake kupata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Dodoma Jiji, mechi ikicheza Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, Taoussi raia wa Morocco, alisema katika mchezo wa jana aliwaambia viungo wake kutochezea sana mpira katikati ya uwanja kutokana na kutokuwa rafiki, badala yake itoke nyuma, kwenda mbele kupita pembeni na kati.

**"Haikuwa mechi rahisi, tulicheza na timu ngumu, nilichogundua kwenye michezo hii ya Ligi Kuu, mifumo na ubora wa wachezaji pekee hautoshi, bali unatakiwa uwe na wachezaji wazoefu na wavumilivu wakiwa uwanjani.**

"Tulipotanguliwa kwa bao moja, niliwaambia wachezaji wangu watulie, na kwa sababu kiwanja hakikuwa rafiki sana niliwaambia wasichezee sana mipira eneo la katikati ya uwanja, hasa viungo, badala yake wairushe mbele na pembeni kwa ajili ya kushambulia mfululizo na hilo limefanikiwa, hii ni mbinu ambayo inatufanya sasa kuwa bora.

"Tunaangalia tucheze mfumo gani kutokana na aina ya kiwanja tunachocheza," alisema kocha huyo ambaye tangu aichukue, Azam FC kutoka kwa Youssouph Dabo, imekuwa kwenye kiwango bora.

Baada ya Yannick Bangala kujifunga dakika ya saba ya mchezo, Nassor Saadun alisawazishia Azam bao dakika ya 11, Feisal Salum akifunga kwa mkwaju wa penalti dakika ya 45, kabla ya Dickson Mhilu wa Dodoma Jiji naye kujifunga dakika ya 60.

Unakuwa ni ushindi wa saba mfululizo kwa Azam FC, tangu ilipolazimishwa suluhu na Mashujaa FC Septemba 29, mwaka huu, Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma.

Baada ya hapo ilianza kutoa vipigo kwa Namungo bao 1-0, ikaichapa Prisons mabao 2-0, ikaikung'uta KenGold 4-1, ikaitandika Yanga 1-0, Kagere Sugar bao 1-0, Singida Black Stars 2-1, kabla ya kushinda tena mechi ya juzi.

Ushindi huo umeipeleka kileleni mwa msimamo wa ligi, ikiiengua Simba kwa kufikisha pointi 30 kwa michezo 13 iliyocheza mpaka sasa.

Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji, Mecky Mexime, alisema waliadhibiwa kutokana na makosa waliyoyafanya, huku wenzao wakitumia faida ya kutumia kila nafasi waliyokuwa wakiipata.




Mshambuliaji wa Azam FC, Nassor Saadun (kushoto), akipongezwa na wachezaji wenzake, James Akaminko na Iddi Nado (kulia), baada ya kuifungia timu yake bao la kusawazisha wakati wakishinda 3-1 dhidi ya Pamba Jiji FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa juzi usiku katika Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza. **MPIGAPICHA WETU**

# *KMC kuongeza mabeki, viungo dirisha dogo*

Na Mwandishi Wetu

KLABU ya KMC imesema ni lazima iingie sokoni kipindi cha dirisha dogo la usajili katikati ya mwezi huu ili kukiongezea nguvu kikosi chake idara ya ulinzi na viungo.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, John Matambala, alisema hayo Jumamosi iliyopita, ikiwa ni siku moja tu baada ya kupata kipigo cha mabao cha mabao 2-0 ilichokipata Ijumaa iliyopita dhidi ya Tabora United kwenye Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam.

Kocha huyo alisema kuna matatizo mengi kwenye sehemu yao ya ulinzi, huku eneo la kiungo wakicheza wachezaji wale wale bila kupumzika, hivyo ni lazima wafanye usajili unaotarajiwa kuanza Desemba 15, mwaka huu.

"Kiukweli dirisha dogo ni lazima watu waongezeke kwenye timu, kwanza ni sehemu ya ulinzi, halafu hata kwenye kiungo mara nyingi wanacheza wale wale tu, ni lazima waje wengine wa kuwasaidia, naamini viongozi wameona na watalifanyia kazi," alisema Matambala.

Akizungumzia mapungufu ya kikosi chake kiasi cha kupoteza michezo mitatu mfululizo, alisema ni kutokuwa na nidhamu wakati hawana mpira.

KMC ilipata kipigo cha mabao 4-0 dhidi ya Simba, 2-1 kutoka kwa Dodoma Jiji, kabla ya Ijumaa kufungwa mabao 2-0 dhidi ya Tabora United.

Alisema timu yake imekuwa ikimiliki sana mpira, lakini inaponyang'anya kunakuwa hakuna nidhamu ya ukabaji wa haraka wa kuzia mianya na wamekuwa wakiadhibiwa kwa hilo.

"Nidhamu ni kitu muhimu sana kwenye soka, vijana wangu wanapambana sana, tatizo nililoliona ni kwamba tunapotea sana tukipoteza mipira, hatuwi makini kukaba wakati wenzetu wakikutana na timu ambayo wanajua kutumia nafasi wanakuadhibu.

"Angalia bao la kwanza kwenye mchezo wetu dhidi ya Tabora United, mchezaji wetu alipoteza mpira wakaanza kwa haraka, hata la pili mpira tulikuwa nao kwa muda mrefu, lakini walipoupata tu wakafanya maamuzi ya haraka," alisema.

Kilikuwa ni kipigo cha pili mfululizo kwa kocha Kalimangonga Ongalla, tangu alipokichukua kikosi hicho kutoka kwa Abduhamid Moallin ambaye sasa ni Mkurugenzi wa Ufundi wa Yanga.

KMC inashika nafasi ya 10 ya msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 14 kwa michezo 13 iliyocheza mpaka sasa.

## Makambo asifu mashabiki wa soka Tanzania

Na Adam Fungamwango

STRAIKA wa Tabora United, Heritier Makambo, amesema amekubali kurudi tena kucheza mpira Tanzania kutokana na kuvutiwa na mashabiki wa soka ambao wanamapenzi makubwa na mchezo huo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam juzi, kabla ya timu kuondoka kurejea Tabora baada ya kucheza mechi ya Ligi Kuu dhidi ya KMC na kushinda mabao 2-1 Ijumaa iliyopita, Uwanja wa KMC Complex uliopo Mwenge, Dar es Salaam, Makambo, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, alisema soka la Tanzania kwa sasa linasifika barani Afrika na sababu kubwa ni mashabiki wengi kujitokeza pale mechi za Ligi Kuu zinapochezwa.

Alisema hata yeye mwenyewe alikubali kurejea nchini alipopata ofa kutoka Tabora United akijua kabisa anakwenda kwenye nchi ya soka.

"Unajua mpira wa Tanzania una msisimko mkubwa kwa sasa barani Afrika kutokana na kuwa na mashabiki wengi. Kwa sasa sehemu kubwa ya Afrika huwezi kuona mashabiki wamejitokeza kwa wingi kama inavyokuwa hapa, na hiki ndicho kitu ambacho nakipenda sana kwenye mpira wa hapa na nilikuwa nikimisi sana, hata nilipopata ofa ya kuja Tabora United nilikubali, kwa kiasi kikubwa nilivutiwa na hilo," alisema straika huyo wa zamani ya Yanga.

Alisema mara nyingi mechi zinapokuwa na mashabiki wengi uwanjani huwapa wachezaji hamu ya kucheza na kupambana.

"Mashabiki wakijitokeza wengi, inawapa wachezaji hamu ya kucheza mpira, kupambana na kuwapambania wanaowashangilia, hiki ni kitu muhimu sana kwenye soka.

"Kwa maana hiyo, nawaheshimu sana na kuwapenda mashabiki wa soka Tanzania, nawaomba waendelee kujitokeza kwa wingi wakati Tabora United inacheza, pamoja na michezo mingine ya Ligi Kuu, ili wachezaji wa kigeni waendelee kumiminika na kusababisha ligi kuendelea kupata umaarufu na hadhi pamoja na kuinua soka la nchi kwa ujumla," alisema Makambo.

Straika huyo mwenye mabao mawili mpaka sasa, alijiunga na Tabora United msimu huu akitokea Al Murooj SC ya Libya, kabla ya hapo alikuwa Klabu ya Yanga, ambayo alikuwa amerejea kwa mara ya pili.

Awali, Yanga ilimsajili akitokea FC Saint Lupopo ya DR Congo mwaka 2019, na 2021 alitimkia Horoya ya Guinea, kabla ya kurejea tena Yanga 2023, lakini hakukaa sana, kwani nusu msimu akaelekea nchini Libya.

## ZISIKUPITE

### PSG KARATA KWA SALAH

KLABU ya Paris St-Germain inajadiliana na mshambuliaji wa Misri, Mohamed Salah, kuhusu uhamisho wa bila malipo wakati mkataba wa mchezaji huyo wa Liverpool mwenye umri wa miaka 32, utakapokamilika mwishoni mwa msimu huu. ***(L'Equipe)***

### GITTENS AFUATILIWA EPL

ARSENAL, Liverpool, Chelsea na Tottenham Hotspur zinamfuatilia mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya England chini ya umri wa miaka 21, Jamie Gittens. ***(Florian Plettenberg)***

### MARMOUSH ANYATIWA

MANCHESTER United, Tottenham Hotspur, Barcelona na Paris St-Germain ziliwatuma wasaka vipaji wao kumfuatilia mshambuliaji wa Misri, Omar Marmoush mwenye umri wa miaka 25, akiichezea Eintracht Frankfurt katika Ligi ya Europa Alhamisi. ***(Mirror)***

### SEMENYO ASAKWA LIVER

KLABU ya Bournemouth iko tayari kupokea ofa ya Antoine Semenyo msimu huu, huku Liverpool wakiwa miongoni mwa klabu zinazomhitaji mshambuliaji huyo wa Ghana mwenye umri wa miaka 24. ***(Football Insider)***

### OLABE KUMRITHI EDU

ARSENAL imepiga hatua katika mazungumzo yao na Roberto Olabe wa Real Sociedad ili kumrithi Edu kama mkurugenzi wa michezo wa Washikabunduki hao. ***(Footmercato)***

### SILVA ATAJWA BRENTFORD

BOURNEMOUTH, Brentford na Southampton zinaitaka saini ya mshambuliaji wa Ureno na Klabu ya Wolves, Fabio Silva mwenye umri wa miaka 22, ambaye yuko Las Palmas kwa mkopo. (***Fichajes)***

### KERKEZ KWA LIVER, UTD

LIVERPOOL inatumaini kuwashinda Manchester United katika usajili wa Januari wa beki wa Hungary, Milos Kerkez mwenye umri wa miaka 21, ambaye Bournemouth imemthaminisha kwa pauni milioni 40. ***(CaughtOffside)***

### TRIPPIER KUWEKWA SOKONI

KLABU ya Newcastle United iko tayari kumuuza beki wa zamani wa England, Kieran Trippier mwenye umri wa miaka 34, katika dirisha la Januari. ***(Football Insider***)


### MOLEIRO AGOMBEWA

AL-Hilal iko tayari kuchuana na Arsenal kwa ajili ya kumsajili winga wa Las Palmas mwenye umri wa miaka 21 raia wa Hispani, Alberto Moleiro. ***(Team Talk)***

### LUTON KULIPA FIDIA

KLABU ya Luton italazimika kulipa pauni milioni 1.5 kumfuta kazi kocha, Rob Edwards kwa sababu ya mkataba wa miaka minne aliosaini msimu wa majira ya joto. ***(Sun)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MO SALAH: HII NI MARA YA MWISHO KUIVAA MAN CITY

**LIVERPOOL,** England

MOHAMED Salah amesema ushindi wa Liverpool wa 2-0 dhidi ya Manchester City itakuwa ni mara ya mwisho kwake yeye kukutana na kikosi cha Pep Guardiola, wakati huu hali ya sintofahamu juu ya mustakabali wake katika klabu hiyo ikiendelea.

**Salah alimtengenezea asisti Cody Gakpo aliyefunga bao la kwanza kwa wenyeji Jumapili kabla ya kufunga penalti kipindi cha pili baada ya Stefan Ortega kumfanyia madhambi Luis Diaz.**

Ushindi huo umeifanya Liverpool kujiimarisha kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu England ikiizidi pointi tisa Arsenal inayoshika nafasi ya pili.

Alipoulizwa kuhusu mustakabali wake baada ya mchezo huo, Salah alikiri kwamba huenda ukawa ndio mwisho wake kukutana na City, huku mkataba wake wa sasa ukitarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu huu.

> Niko nje zaidi kuliko ndani, hakuna klabu kama hii, lakini mwisho hauko mikononi mwangu...

Akizungumza na Sky Sports, Salah alisema: "Kusema kweli hadi sasa huu ni mchezo wa mwisho dhidi ya City kuichezea Liverpool, kwa hiyo nilikuwa naenda kufurahia tu. Hali ilikuwa ya ajabu hivyo nitafurahia kila sekunde hapa. Natumaini tutashinda ligi tu na tutaona kitakachotokea."

Ni mara ya pili katika kipindi cha siku nane ambapo Salah amezungumza kuhusu mustakabali wake, baada ya kusimama kuzungumza na waandishi wa habari kutokana na ushindi wa Liverpool wa mabao 3-2 dhidi ya Southampton wikendi iliyopita.

"Sawa, karibu Desemba na sijapokea ofa yoyote ya kubakia kwenye klabu, hivyo huenda niko nje zaidi kuliko ndani," alisema Salah baada ya ushindi huo kwenye Uwanja wa St. Mary's.

"Unajua sasa nimekuwa kwenye klabu kwa miaka mingi, hakuna klabu kama hii, lakini mwisho hauko mikononi mwangu. Kama nilivyosema hapo awali, ni Desemba na sijapokea chochote kuhusu maisha yangu ya baadaye.

"Nawapenda mashabiki. Mashabiki wananipenda. Mwisho uamuzi haupo mikononi mwangu au mikononi mwa mashabiki. Hebu tusubiri tuone."

Chanzo kimoja kiliiambia ESPN kwamba mazungumzo kati ya wawakilishi wa Salah na Liverpool yamekuwa yakiendelea na mazuri, ingawa mazungumzo yake ya mkataba yalitarajiwa kuwa magumu na kuchukua muda.

Salah alisaini mkataba wake wa mwisho na Liverpool, ambao ulimfanya kuwa mchezaji anayelipwa fedha nyingi zaidi katika klabu hiyo, Juni 2022.

# GUARDIOLA: MAN CITY ITAANZA UPYA



**LIVERPOOL,** England

PEP Guardiola amesema Manchester City lazima sasa "ianze upya kutoka sifuri" baada ya kipigo cha mabao 2-0 kutoka kwa Liverpool na kumfanya apoteze katika mechi sita mfululizo.

Mabao kutoka kwa Cody Gakpo na Mohamed Salah yaliihakikishia Liverpool ushindi ambao walisonga mbele kwa pointi tisa kileleni mwa jedwali. City imebakia nafasi ya tano.

Guardiola alikejeliwa kwa sauti za "unafukuzwa asubuhi" na mashabiki wa Liverpool na kocha huyo alijibu kwa kuonesha vidole sita kwa umati kuashiria idadi ya mataji aliyoshinda wakati alipokuwa Etihad - na alikiri baada ya mchezo kwamba hali ya unyonge ya kushindwa huko Anfield ina maana kwamba City lazima sasa "ianze upya."

"Ninawapongeza Liverpool na tutarejea na kuanza kutoka sifuri na ni vigumu kuamini," alisema Guardiola.

"Tutaanza upya na kujaribu kufanya jambo.

"Tunakubali ukweli jinsi ulivyo na kupona. Nataka timu irudi, wachezaji warudi.

"Nawategemea sana wachezaji hawa, najua wanafanya katika nafasi hii, tutaona kitakachotokea mwishoni mwa msimu. Nina hisia kutoka hapa kwamba tunaweza kujenga kitu, labda unaweza kuniita muongo, lakini ninahisi tunaweza kuifanya.

"Dakika 15, 20 za kwanza Liverpool walikuwa hawazuiliki, walianza kwa nguvu sana, tulijaribu kucheza kwa udhibiti na pasi nyingi, lakini ilikuwa ngumu kuipokea."

Guardiola, ambaye alitia saini mkataba mpya wa miaka miwili Novemba, ana imani kuwa wachezaji hao watageuza hali hiyo kurudia mafanikio ya awali.

# Mbappe sasa amkuna Ancelotti

**MADRID,** Hispania

CARLO Ancelotti alimsifu Kylian Mbappe kuwa "hatari" baada ya kufunga bao zuri katika ushindi wa 2-0 wa Real Madrid dhidi ya Getafe Jumapili, akisema "hilo ndilo tunalotaka kutoka kwake" baada ya fowadi huyo kukosolewa kwa uchezaji wake hivi karibuni.

Jude Bellingham aliiweka Madrid mbele kwa mkwaju wa penalti dakika ya 30, kabla ya kumtengenezea Mbappe bao la pili dakika nane baadaye.

Matokeo hayo yameiweka Madrid nyuma kwa pointi moja dhidi ya vinara Barcelona, wakiwa na mchezo mmoja mkononi.

"Mbappe alikuwa hatari kama kawaida," alisema Ancelotti katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi.

"Alifunga bao muhimu kutusaidia kudhibiti mchezo vema, na alipata nafasi katika kipindi cha pili. Alikuwa na mchezo mzuri sana, na hilo ndilo tunalotaka kutoka kwake."

Mbappe alikuwa amefunga mabao mawili pekee katika mechi tisa kabla ya mechi ya Jumapili kwenye Uwanja wa Santiago Bernabeu - na alikosa penalti dhidi ya Liverpool kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya katikati ya wiki.

"Ilikuwa ahueni," alisema Ancelotti.

"Kwa 2-0, una nafasi zaidi ya kushinda... lilikuwa bao la kuvutia na la kustaajabisha. Mchezo wa Mbappe ulikuwa mzuri sana.

"Mashabiki wanaelewa zaidi kuliko mtu mwingine yeyote wakati wa timu na wachezaji ni nini. Walimuunga mkono Mbappe kitu ambacho ni sawa."

Madrid itasafiri kuifuata Athletic Club kwenye LaLiga Jumatano, na kisha Girona Jumamosi, kabla ya kurejea uwanjani kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Atalanta.

# *Amorim aitoa Manchester Utd nne bora*



**MANCHESTER,** England

RUBEN Amorim amepuuza uwezekano wa Manchester United kumaliza katika nafasi nne za juu za Ligi Kuu msimu huu licha ya kuiongoza timu yake kushinda 4-0 dhidi ya Everton Jumapili.

United waliingia nusu ya kwanza ya msimamo kutokana na mabao mawili ya kila mmoja Marcus Rashford na Joshua Zirkzee kwenye Uwanja wa Old Trafford.

Man United sasa imejikita nafasi ya tisa kwenye msimamo na Amorim alikataa kukubali kwamba, wanaweza kumaliza ligi wakiwa ndani ya nne bora.

"Nikisema hapana utasema siwezi kuwa kocha wa Manchester United, lakini nataka kuwa mkweli kwa mashabiki wetu," alisema Amorim.

"Tuzingatie uchezaji na si matokeo, tutaona mwisho, nitapimwa sehemu ambayo tutamaliza, najua hilo, tujikite kwenye mchezo ujao.

"Kwa hiyo tuzingatie uchezaji. Hongera vijana. Tupumzike na tupate nafuu na kuifikiria Arsenal."

Zirkzee alikuwa chaguo la kushtukiza dhidi ya Everton, lakini alilipa imani ya Amorim kwa mabao yake ya kwanza ya United tangu Agosti, mwaka huu.

Rashford, kwa sasa amefunga mabao matatu katika mechi tatu chini ya kocha huyo mwenye umri wa miaka 39, baada pia kufunga katika mchezo wake wa kwanza dhidi ya Ipswich.

"Yeye (Rashford) anaweza kufanya mengi," alisema Amorim, ambaye sasa ataipeleka timu yake pale kwenye dimba la Emirates kucheza na Arsenal Jumatano.

"Lazima aendelee kuimarika, ana uwezo wa kufanya hivyo na tayari amethibitisha hilo. Lakini anaweza kucheza vizuri zaidi kama wachezaji wengine kwa hiyo ulikuwa ni mchezo mzuri."

HABARI MICHEZO

## Fadlu ataka kila mchezaji Simba kufunga

INATOKA UK. 24

ya CS Constantine, unaotarajiwa kupigwa Jumapili saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Mohamed Hamlaoui, alisema yanaenda vizuri na wamejiandaa kukabiliana na timu hiyo.

"Katika hatua ya makundi hakuna timu rahisi, tunakwenda kucheza mchezo mgumu ugenini, lakini malengo yetu yapo pale pale, ama kushinda au ikishindikana kutoa sare," alisema.

Fadlu pia alionekana kufurahishwa na ujio wa mchezaji Elie Mpanzu ambaye ataanza kutumikia timu hiyo kuanzia Desemba 15, mwaka huu akisema atasaidia sana kwenye mechi zijazo za kimataifa baada ya mchezo wa Jumapili.

"Nadhani kutakuwa na maingizo mapya machache, akiwamo Mpanzu, huyu tayari namfahamu, tunafanya naye mazoezi, ni mchezaji mzuri kwa kweli, anaweza kucheza winga zote mbili, ana uwezo wa kucheza nyuma ya mshambuliaji, yeye mwenyewe binafsi anaweza kufanya kitu kitokee, anaweza kubaki na mabeki mmoja au wawili akavuruga wote, ataingiza kitu kipya kwenye kikosi chetu," alisema Fadlu, raia wa Afrika Kusini.

Kama mambo yatakwenda kama yalivyopangwa kwa mujibu wa uongozi wa Simba, kikosi hicho kinatarajiwa kuondoka Jumatano kwenda mji wa Constantine, Algeria ambako mchezo huo utafanyika.

## Yanga mzuka juu Ligi ya Mabingwa

INATOKA UK. 24

niwaambie kuwa waendelee kutusapoti na hatutowaangusha tena," alisema Abuya winga na kiungo mshambuliaji wa timu hiyo ambaye tangu aje kocha Sead Ramovic amekuwa akimtumia kama kiungo mkabaji.

Yanga ilianza kwa kichapo cha bao 1-0 kwenye mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Azam FC, uliochezwa Novemba 2, mwaka huu, katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, kabla ya kuchapwa mabao 3-1 dhidi ya Tabora United Novemba 7, mwaka huu kwenye uwanja huo huo, na Jumanne iliyopita, ilifungwa mabao 2-0 dhidi ya Al Hilal Omdurman ya Sudan katika mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi, uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

# PAMBA YAPIGWA FAINI MIL. 5/- KISA SIMBA, MINZIRO ATAMBA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya ushindi wa bao 1-0 dhidi ya KenGold juzi, katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliopigwa Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza, Kocha Mkuu wa Pamba Jiji, Fred Felix Minziro, amesema sasa gari limewaka, huku klabu hiyo ikitozwa faini ya Sh. milioni tano kwa kosa la baadhi ya maofisa wake kuingilia mazoezi ya timu ya Simba.

Akizungumza baada ya mechi hiyo, alisema ushindi huo, ukijumlisha na uliopita walivyoifunga Fountain Gate mabao 3-1 kwenye Uwanja wa Tanzanite Kwaraa, Babati mkoani Manyara, na kufungwa kwa kwa tabu bao 1-0 dhidi ya Simba Novemba 22 , mwaka huu, Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza, inaonesha kuwa kikosi chake kimeimarika kwa kiasi kikubwa tofauti na kilivyoanza ligi.

**"Nadhani sasa tumeimarika si kama tulivyoanza ligi, nimeendelea kukiimarisha siku hadi siku, matokeo ya hivi karibuni yanaonesha hilo, tumebakisha michezo miwili tumalize mzunguko wa kwanza, nadhani huko mbele hatutokuwa hivi tena, tutaendelea kuimarika zaidi," alisema kocha huyo.**

Akiuzungumzia mchezo huo alisema haukuwa rahisi, lakini anawashukuru vijana wake kwa kupambana na kupata ushindi huo uliowasogeza juu kidogo ya msimamo.

"Mechi haikuwa rahisi, presha ilikuwa juu, nawashukuru vijana wangu kwa kupambana hadi tumepata ushindi ambao utawafanya warudishe morali na kujiamini zaidi katika michezo ijayo," alisema.

Kocha Mkuu wa KenGold, Omari Kapilima, alisema matokeo hayo hakuyatarajia, kwani alijipanga kushinda au kupata sare ugenini.

"Matokeo sikuyatarajia, lakini ni moja ya matokeo ya mchezo wa soka. Nilipanga mipango ambayo haikukubali, nikabadilisha wachezaji watatu kipindi cha kwanza, hata hivyo haikusaidia tukapoteza kwa bao 1-0, bado nina kazi ya kufanya kwenye mazoezi kurekebisha hali hii," alisema.

Matokeo hayo yanaifanya Pamba Jiji kupanda hadi nafasi ya 12 ya msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa na pointi 11 kwa michezo 13 iliyocheza, huku KenGold, ikiburuza mkia ikiwa na pointi sita kwa michezo 13 iliyocheza mpaka sasa. Timu zote hizo zimebakisha michezo miwili kila moja ili kumaliza mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu msimu huu.

Wakati huo, klabu hiyo imetozwa faini kiasi cha Sh. milioni tano, baada ya baadhi ya maofisa wake kuingilia mazoezi ya timu ya Simba siku moja kabla ya mchezo baina yao uliochezwa, Uwanja wa CCM Kirumba, Novemba 22, mwaka huu Wekundu wa Msimbazi walipondoka na ushindi wa bao 1-0.

Taarifa iliyotolewa jana na Bodi ya Ligi, imesema maofisa wa timu hiyo walionekana uwanjani katika muda wa kikanuni wa timu hiyo kufanya mazoezi.

Bodi imesema maamuzi hayo yamefanywa na Kamati ya Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania Bara (TPLB).

UMETISHA...




Mshambuliaji wa Manchester United, Joshua Zirkzee (wa pili kulia), akipongezwa na wachezaji wenzake baada ya kuifungia timu yao bao la nne na pili kwake katika mechi ya Ligi Kuu England dhidi ya Everton wakati wakishinda 4-0 kwenye Uwanja wa Old Trafford juzi. **PICHA: MTANDAO**

# Mabao yakujifunga yaongezeka Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

MABAO mawili ya kujifunga katika mchezo wa juzi wa Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Dodoma Jiji na Azam FC, yameongeza idadi ya mabao ambayo wachezaji wamejifunga wenyewe kufika manne kwenye michezo 97 iliyochezwa mpaka sasa.

Mechi ya juzi, imeweka rekodi ya wachezaji wawili kujifunga wenyewe kwenye mchezo mmoja.

Katika mechi hiyo, iliyochezwa, Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, kiungo mkabaji wa Azam FC, Yannick Bangala, alijifunga mwenyewe dakika ya saba ya mchezo na kuipa Dodoma Jiji bao la kufutia machozi kwenye mchezo huo ambao Wanalambalamba walishinda kwa mabao 3-1.

Beki wa Dodoma Jiji, naye alijifunga dakika ya 60 katika jitihada zake za kutaka kuokoa, akiipa Azam FC bao la tatu kwenye mechi hiyo, timu yake ikipokea kipigo cha mabao 3-1.

Mchezaji wa kwanza kujifunga kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu ni Fred Tangalo wa KMC, akifanya hivyo Septemba 19, mwaka huu, katika mchezo kati ya timu yake na Azam FC, ukipigwa Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam.

Katika mchezo huo ambao Azam ilishinda mabao 4-0, moja kati ya hilo lilikuwa la KMC kujifunga wenyewe kupitia kwa beki huyo.

Beki wa kulia wa Simba, Kevin Kijili alijifunga, Oktoba 19, mwaka huu, katika mchezo kati ya timu yake na Yanga, uliochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, na lilikuwa bao pekee, Yanga ikishinda 1-0.

Kwa mujibu wa Kitengo cha Takwimu na Rekodi cha Dawati la Michezo la Nipashe, jumla ya mabao 192 yamefungwa mpaka sasa kwenye Ligi Kuu katika michezo 97 iliyochezwa, 20 yakifungwa kwa mikwaju ya penalti, manne yakiwa ya kujifunga.

# Michezo

Jumanne Desemba 3, 2024

Nipashe




Mbappe amkuna Ancelotti UKURASA 22

TULIA...



Winga wa kushoto wa Liverpool, Luis Diaz, katika harakati za kufumania nyavu huku akipata upinzani mkali kutoka kwa beki wa kulia wa Manchester City, Kyle Walker (kulia), kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Anfield juzi usiku. Liverpool ilishinda 2-0.
**PICHA: MTANDAO**

## Fadlu ataka kila mchezaji Simba kufunga mabao

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amesema anatengeneza mfumo ambao utawawezesha wachezaji wake wote kuweza kufunga mabao au kutoa pasi za mwisho kwa manufaa ya timu na si kutegemea mastraika kufunga au mchezaji mmoja kutoa pasi ya mwisho 'asisti.'

Akizungumza juzi jijini Dar es Salaam wakati wa maandalizi ya mchezo wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya CS Constantine unaotarajiwa kucheza nchini Algeria Jumapili wiki hii, Fadlu alisema mafanikio ya timu hayawezi kuletwa na mchezaji mmoja pekee yake, hasa kufunga mabao, hivyo anatengeneza mfumo utakaomwezesha kila mchezaji kuanzia mabeki, viungo mpaka washambuliaji kupachika mipira ndani ya wavu.

"Natengeneza kikosi ambacho kitakuwa na ushirikiano, kitacheza kama timu, mafanikio hayawezi kumtegemea mchezaji mmoja ndiyo afunge mabao, kila mmoja anatakiwa achangie ushindi, ni golikipa tu ndiyo kazi yake itakuwa ni kuzuia mabao yasiingie wavuni kama alivyofanya Moussa Camara katika mchezo dhidi ya Bravo do Maquis, waliobaki wote pamoja na majukumu yao mengine, lakini wanatakiwa wachangie 'asisti' na kufunga mabao pia," alisema kocha huyo.



Alisema mbinu na mfumo huo lengo lake ni kuleta tija katika kupata mabao mengi zaidi kwenye mchezo ili kuleta maendeleo kwenye kikosi chake.

Fadlu alisema hayo siku kadhaa timu yake ikitoka kucheza mchezo wa kwanza hatua ya makundi Kombe la Shirikisho dhidi ya Bravo do Maquis, ikishinda bao 1-0, ambapo baadhi ya wadau wa soka na mashabiki wanadai kulikuwa na viashiria kwa uchoyo kwa baadhi ya wachezaji kunyimana pasi kwenye maeneo muhimu, huku kila mmoja akipata mpira akionekana kutaka kuamua mchezo mwenyewe.

Akizungumzia maandalizi ya mchezo dhidi

INAENDELEA UKURASA 23

# Yanga mzuka juu Ligi ya Mabingwa

**Na Adam Fungamwango**

● ● ● Wachezaji wasema wametua mzigo mzito kichwani ushindi dhidi ya Namungo, hivyo wanakwenda Algeria wakiwa...

WACHEZAJI wa Yanga wamekiri kuwa walikuwa kwenye wakati mgumu baada ya kupoteza michezo mitatu mfululizo, kitu ambacho si cha kawaida kwa timu kubwa kama hiyo.

Wakizungumza jijini Dar es Salaam juzi baada ya kutoka mkoani Lindi ilipokwenda kucheza dhidi ya Namungo na kushinda mabao 2-0 katika Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa, kwa mara ya kwanza baada ya kupoteza michezo miwili mfululizo ya Ligi Kuu na mmoja wa Ligi ya Mabingwa Afrika, wachezaji hao walisema ushindi huo umewapa faraja na kuwarudisha kwenye matumaini ya kufanya vema kwenye michezo ijayo.

**Nahodha Msaidizi, Dickson Job, alisema kulikuwa na presha ndani ya timu baada ya matokeo mabovu, lakini ushindi dhidi ya Namungo umeondoa kila kitu na sasa wanaangalia mbele, hasa katika mchezo wao wa Jumamosi dhidi ya MC Alger nchini Algeria.**

"Mchezo dhidi ya Namungo haukuwa rahisi kama watu walivyodhani, ulikuwa mgumu kwa sababu kuna presha ambayo ilianza kuingia kwenye timu baada ya kupoteza mechi zetu mbili za Ligi Kuu na ile ya kimataifa dhidi ya Al Hilal.

"Kikubwa kupoteza michezo ile maana yake tulikuwa nje ya malengo, lakini wachezaji tulitulia na kuangalia nini kinahitajika ili turejeshe makali yetu, kweli tumefanya hivyo na tumeshinda dhidi ya Namungo, ushindi ambao umetuweka vizuri sasa kuelekea kwenye mchezo wetu wa Jumamosi," alisema Job, anayemudu kucheza beki wa pembeni na kati.

Yanga itacheza mechi ya pili ya Ligi ya Mabingwa Afrika Jumamosi ijayo kwenye Uwanja wa Juillet wa Tano jijini Algiers nchini Algeria, saa 4:00 usiku kwa saa za Tanzania.

Mchezaji mwingine, Duke Abuya, alisema ushindi walioupata unakwenda kwa mashabiki na kuwaomba msamaha baada ya kuwapa huzuni na kuwavunja nguvu, akiahidi kuwa hilo halitatokea tena la kupoteza michezo mitatu mfululizo.

"Tulikuwa kwenye wakati mgumu sana, kupata huu ushindi kimekuwa kitu cha maana sana, kimeturudisha wachezaji kwenye msitari.

"Nawaomba wachezaji wenzangu tuendelee na mwendelezo huu, tumewavunja nguvu na kuwahuzunisha mashabiki wetu, lakini sasa tuwafanye warudishe furaha yao walioizoea,


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >